**Shamila:** Kila siku, mimi hufika chuoni mapema sana. Kisha, mimi huenda darasani na husoma vitabu vya hadithi. Baada ya kusoma, mimi huenda maktabani kufanya utafiti, na huhudhuria semina kwenye idara. Baadaye, mimi na rafiki zangu hutazama soka katika uwanja wa chuo.

**Farida:** Baada ya kutazama soka wewe hufanya nini?

**Shamila:** Mimi hufanya kazi ya nyumbani, husikiliza Muziki, hurudi nyumbani na hupumzika. Na wewe hufanya nini kwa kawaida kazini?

**Farida:** Katika ofisi, mimi hupokea simu, hupanga ratiba ya mikutano, huhudhuria mikutano mbalimbali, hukagua miradi, huandika na kujibu barua pepe. Wakati wa chakula cha mchana mimi humtembelea rafiki yangu. Jioni, mimi huenda sokoni kununua bidhaa na hurudi nyumbani. Mara moja kwa wiki mimi huhudhuria mkutano wa chama cha wanawake pamoja na rafiki zangu.

**Shamila:** Inaonekana, wewe huwa na shughuli nyingi kila siku. Wewe hupumzikaje?

**Farida:** Mimi hupenda kupumzika kwa kutazama filamu.

**Shamila:** Mimi pia. Usiku mwema.

**Farida:** Usiku mwema pia.

1. Shamila hufanya shughuli gani chuoni kila siku?
2. Shamila hufanya nini baada ya kutazama soka?
3. Bibi Farida hufanya nini ofisini?
4. Baada ya kazi, Bibi Farida hufanya nini?
5. Shamila na Bibi Farida hupenda kufanya nini wakati wa kupumzika?
6. Wewe unapenda kufanya shughuli gani kila siku?



### Zoezi M

One of your classmates is looking for a hiking partner on the weekends. They want to plan for a two-day hike on Mt. Meru in Arusha and would like to see if you can come along. In the information exchange, give your classmate your typical weekend schedule and inform them if you will be able to join them.



### Zoezi N

One Saturday morning, Shamila came across a podcast focused on strategies for keeping up with housework. In the current episode, the speaker Malaika Msafi discusses her major household activities as a homemaker. Listen to the podcast and answer the questions that follow.

1. Bibi Malaika anazungumza kuhusu nini?
2. Kwa nini Bibi Malaika husafisha nyumba yake wikendi?
3. Bibi Malaika hufanya shughuli gani Jumamosi?
4. Baada ya kusafisha nyumba Bibi Malaika hufanya nini?
5. Bibi Malaika, hufanya nini baada ya kula chakula cha jioni?
6. Bibi Malaika huwalisha watoto wakati gani?
7. Kabla ya kupika chakula cha jioni, Bibi Malaika hufanya nini?
8. Kwa nini Bibi Malaika hupiga nguo pasi kabla ya kulala?
9. Wewe hufanya nini kila wikendi?

## Vocabulary: Siku za Wiki (*Days of the Week*)

The days of the week are drawn from the Muslim weekly pattern of worship in which *Jumamosi* (Saturday) is considered the first day of the week. Friday is the main day of worship and is thus the last day of the week in the calendar. Most of the days of the week in Kiswahili are formed by combining the root of the word *juma* (week) with the number in the weekly calendar on which the day falls. For instance, *Jumamosi* is a combination of *juma* and numeral *mosi* (one).

Je, leo ni siku gani?

*What day is it today?*

**Leo ni siku** ya Jumanne.

**Today is** Tuesday.

Mimi huenda darasani siku ya **Jumanne**. *I go to class on **Tuesdays**.*

You might already know that most American calendars start the week with Sunday as the first day while other countries, France for example, begin their week on Monday. This difference indicates that calendars are influenced by regional factors, religion among others. For Kiswahili speakers, the first day of the week is Saturday. While most calendars in East Africa are in English, a Swahili calendar looks like this:



## NOVEMBA

Jumapili	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30			



## Zoezi O

Work with a classmate and take turns asking each other the day of the week. Next, randomly select a date on the calendar and ask your classmate to name the day of the week.

### **Examples:**

Leo ni siku gani?

Tarehe ishirini na nne ni siku gani ya wiki?

Tarehe ishirini na nne ni siku ya Jumatatu.

*What day is today?*

*What day of the week is the 24<sup>th</sup>?*

*The 24<sup>th</sup> is a Monday.*



## Zoezi P

Shamila and Joseph talk about what they do on different days of the week. Read their conversation and answer the questions that follow.

**Shamila:** Habari za mchana?

**Joseph:** Nzuri sana. Na wewe je?

**Shamila:** Nzuri tu. Je, wewe huenda chuoni siku gani?

**Joseph:** Mimi huenda chuoni Jumatatu, Jumanne, na Jumatano. Na wewe je?

**Shamila:** Mimi huenda chuoni Jumatatu, Jumatano na Ijumaa.

**Joseph:** Wewe hufanya nini siku ya Jumanne na Alhamisi?

**Shamila:** Mimi hufanya kazi ya kujitolea katika shule ya sekondari ya Matunda. Wewe hufanya nini siku ya Ijumaa?

**Joseph:** Mimi hufanya kazi ya nyumbani, kisha huenda msikitini kwa sala za Ijumaa pamoja na familia yangu.

**Shamila:** Wewe hufanya nini siku ya Jumamosi na Jumapili?

**Joseph:** Mimi hupumzika sana wikendi. Mimi hutazama filamu, huzungumza na familia yangu Marekani, huenda sokoni na huenda matembezi katika sehemu mbalimbali hapa Tanzania. Na wewe je?

**Shamila:** Jumamosi mimi huzungumza na familia yangu, huenda ziara mjini, hutembelea rafiki na huenda ufukweni. Jumapili mimi huenda na familia yangu kanisani.

1. Shamila huenda chuoni siku gani?
2. Joseph huenda chuoni siku gani?
3. Je, Joseph huenda kanisani siku ya Jumapili?
4. Familia ya Shamila hufanya nini wikendi?
5. Shamila hufanya nini siku ya Jumanne na Alhamisi?



### Zoezi Q

You would like to find a Kiswahili study partner among your classmates. Interview three classmates to find out what they do on different days of the week. Let your classmates know what you do on different days of the week as well. Report to the class which classmates you might prefer to plan your study time with based on what they do on different days. Give the reasons for your selection.



### Zoezi R

Poll your classmates to find out how often they engage in activities that are popular among college students and report back on what you find out.



### Zoezi S

Listen to the telephone conversation between Juma and Bakari and provide details about the frequency of their daily activities in the space provided below.

#### **Bakari**

- 1.
- 2.
- 3.
- 4.

#### **Juma**

- 1.
- 2.
- 3.
- 4.

## Key Vocabulary

### *Words of Frequency*

<b>awali</b>	fast; origin
<b>baada ya</b>	after; afterwards
<b>baadaye</b>	later
<b>chelewa</b>	late
<b>halafu</b>	afterwards; then
<b>kila wakati</b>	all the time
<b>kwa kawaida</b>	normally; usually
<b>kwa muda mfupi</b>	for a short time
<b>kwa muda mrefu</b>	for a long time
<b>mapema</b>	early
<b>mara kwa mara</b>	from time to time
<b>mara (mbili) kwa mwezi</b>	twice a month
<b>mara (moja) kwa (wiki)</b>	once a week
<b>mara mojamoja</b>	once in a while
<b>mpaka; hadi</b>	until
<b>mwanzo</b>	start; begin; genesis
<b>mwishowe</b>	finally
<b>nadra</b>	rarely
<b>zamani</b>	past

### *Conjunctions*

<b>au; ama</b>	or
<b>badala ya</b>	instead of
<b>bila</b>	without
<b>ijapo</b>	even if
<b>ila</b>	except
<b>ingawa</b>	even though
<b>juu ya hayo</b>	moreover
<b>kama</b>	if; like
<b>kisha</b>	then; moreover
<b>kwa</b>	for; to; by; with
<b>kwa sababu</b>	because
<b>lakini</b>	but
<b>tena</b>	again
<b>wakati wa</b>	during; while

### *Nouns*

<b>asubuhi</b>	morning
<b>baa</b>	bar
<b>bahari</b>	ocean
<b>barua pepe</b>	email
<b>bidhaa</b>	products; goods
<b>bweni</b>	dormitory
<b>chai</b>	tea
<b>chumba cha kula</b>	dining hall
<b>chumba cha mazoezi</b>	gym
<b>chuoni</b>	college

**dansi** dance  
**darasa** classroom  
**duka** shop  
**duka la dawa** pharmacy  
**duka la vitabu** bookstore  
**filamu** film; movie  
**gazeti** newspaper  
**jarida** journal; magazine  
**jioni** evening  
**kahawa** coffee  
**kanisa** church  
**kituo cha basi** bus stop  
**maktaba** library  
**mchana** daytime  
**meza ya lugha** language table  
**mkahawa** restaurant  
**mkutano** meeting  
**mradi** project  
**msala** restroom  
**msikiti** mosque  
**muziki** music  
**ofisi** office  
**pwani** coast  
**raga** rugby  
**Sala za Ijumaa** Friday prayers  
**sehemu** part; side  
**siku** day  
**siku za wiki** day(s) of the week  
**simu** cell phone  
**soko** market  
**tarehe** date (*day of the month*)  
**ufukwe** beach; shore  
**ujumbe mfupi** short text message  
**usiku** night  
**utafiti** research  
**uwanja** court; field (*for sports*)  
**vitabu vya hadithi** storybooks  
**wikendi** weekend  
**wiki** week  
**ziara** tour; visit  
**ziwa** lake

*Days of the week*

**Jumapili** Sunday  
**Jumatatu** Monday  
**Jumanne** Tuesday  
**Jumatano** Wednesday  
**Alhamisi** Thursday  
**Ijumaa** Friday  
**Jumamosi** Saturday



## Verbs

- angalia tovuti** to look at the internet; to surf the web
- enda kwa mkutano** to go to a meeting
- enda matembezi** to go for a walk
- endelea** to go on; to move along
- fanya kazi ya kujitolea** to do volunteer work
- fanya marudio** to do review
- fanya mazoezi** to exercise
- fanya utafiti** to do research
- fika** to arrive
- fundisha** to teach
- hudhuria mkutano** to attend a meeting
- jibu barua pepe** to respond to email
- kagua** to check; to inspect
- ogelea** to swim
- piga chapa** to type
- pokea simu** to receive a phone call
- safisha vyombo** to wash the dishes
- sikiliza musiki** to listen to music
- tengeneza** to make; to prepare
- weza** to be able to
- zungumza** to talk; to speak

## Key Phrases

- huwa na shughuli** to be busy
- huwa na shughuli chache** to be less busy
- huwa na shughuli nyingi** to be very busy
- huwa sina shughuli** to not be busy
- Kuanzia...** To start with...
- kutoka saa (moja) hadi saa (nne)** from (1 o'clock) until (4 o'clock)
- Kutoka siku ya...** From the day of...
- Leo ni siku gani?** What day is today?
- Leo ni siku ya...** Today is...
- ...mara ngapi kwa (wiki)?** ...how many times per (week)?
- Siku gani...?** Which day...?
- Usiku mwema!** Have a good night!

### 3.3 Kusema wakati



saa saba (kamili)



saa nane na robo



saa tisa na nusu



saa kumi na moja  
kasorobo



#### Zoezi A

Shamila describes her daily schedule with her host family to Joseph and other classmates. Read her description and answer the questions that follow.



Hamjambo wanafunzi wenzangu?

Habari za leo? Mimi ninafurahi sana kuishi pamoja na familia yangu pokezi. Sisi hufanya vitu vingi pamoja na wao hunisaidia kila mara. Kwa kawaida mimi huamka saa kumi na mbili na nusu asubuhi. Hutandika kitanda, huoga, hupiga nguo pasi, huvaa nguo na mapambo. Mimi humsaidia Bibi Farida kuandaa chakula cha asubuhi. Sisi hula chakula cha asubuhi saa mbili na nusu asubuhi. Mimi huenda chuoni kutoka saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni. Nikiwa chuoni mimi huenda darasani, huenda maktabani kufanya utafiti na hushiriki katika meza ya Kiswahili. Mimi hurudi nyumbani kati ya saa kumi na mbili jioni na saa moja na nusu usiku. Mimi hula chakula cha jioni saa tatu usiku, humsaidia Bibi Farida kusafisha vyombo, kisha sisi hupumzika kwa kutazama televisheni pamoja. Mimi hulala kati ya saa nne na nusu na saa tano usiku.


Is it true (*kweli*) or false (*si kweli*)? If false, make the necessary changes to create a true statement.

1. Baada ya kuamka, Shamila hupiga mswaki, hufua nguo, na husafisha chumba.
2. Shamila huwa haandai chakula cha asubuhi na Bibi Farida.
3. Familia ya Bibi Farida hula chakula cha asubuhi saa kumi na mbili na nusu asubuhi.
4. Shamila huenda darasani na maktabani akiwa chuoni.
5. Shamila hulala saa sita za usiku.
6. Shamila hurudi nyumbani kati ya saa kumi na mbili jioni na saa moja na nusu usiku.
7. Baada ya chakula cha jioni Shamila husafisha vyombo pamoja na Bibi Farida.
8. Kabla ya kulala Shamila huzungumza kwa simu.



### Zoezi B

Farida describes Joseph's schedule to a guest who is visiting. Read her description and answer the questions that follow.



Joseph ni mwanafunzi wa chuo kikuu na atakaa na sisi kwa muda wa mwaka mmoja. Kwa sasa yeye ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yeye hufanya shughuli mbalimbali kila siku. Kutoka Jumatatu hadi Ijumaa, yeye huamka mapema kila siku. Yeye huamka saa kumi na mbili kamili asubuhi. Yeye huondoka nyumbani saa tatu kamili asubuhi kwa sababu yeye huhudhuria madarasa kutoka saa nne asubuhi hadi saa kumi na nusu jioni. Yeye hufanya utafiti mtaani kwa saa tatu mara tatu kwa wiki siku za Jumatatu, Jumatano na Alhamisi kutoka saa kumi na nusu jioni hadi saa moja na nusu usiku. Yeye hurudi nyumbani kabla ya saa tatu za usiku. Yeye hula hutazama televisheni na

huzungumza kwa simu kabla ya kulala. Wikendi yeye huwa hafanyi vitu vingi. Yeye hupumzika sana, hutembelea miji mbalimbali, hupenda kwenda ufukweni pamoja na rafiki zake wapya, na hushiriki katika shughuli za kitamaduni na familia yetu.

1. Joseph huwa na shughuli za utafiti siku gani na saa ngapi?
2. Joseph huhudhuria madarasa siku gani?
3. Joseph hurudi nyumbani saa ngapi?
4. Joseph hufanya nini wikendi?
5. Wewe huhudhuria madarasa yako siku gani na saa ngapi?
6. Kutoka siku ya Jumatatu hadi Ijumaa wewe huamka saa ngapi?
7. Wikendi wewe huamka saa ngapi?

### **Sarufi: Kusema wakati (*Stating time*)**

In East Africa, the system of telling time differs from that of western countries. The hour of the day is based on the number of hours after the sunrise and sunset rather than the number of hours after midnight (a.m.) and noon (p.m.)



**saa moja za asubuhi**  
(*first hour of the day*)  
OR  
**saa moja za usiku**  
(*first hour of the night*)



**saa sita za mchana**  
(*sixth hour of the day*)  
OR  
**saa sita za usiku**  
(*sixth hour of the night*)

When telling time, one can say either *saa moja za asubuhi* or *saa moja asubuhi*. The time of the day (e.g., *asubuhi, mchana, jioni, usiku, alfajiri*, etc.) needs to follow the time.

The day is subdivided as follows:



**asubuhi**

7:00 a.m.

-

11:59 a.m.



**mchana**

12:00 p.m.

-

3:59 p.m.



**jioni**

4:00 p.m.

-

6:59 p.m.



**usiku**

7:00 p.m.

-

3:59 a.m.



**alfajiri**

4:00 a.m.

-

6:59 a.m.

Here are a few other useful words and phrases for telling time:



saa moja na **dakika ishirini**  
**asubuhi/usiku**  
(seven twenty **a.m./p.m.**)

saa = time; hour

dakika = minute(s)

sekunde = second(s)

nusu = half past

kamili = on the hour/exact

kasorobo = quarter to

robo = quarter past/after



## Zoezi C

*Ni saa ngapi?* (What time is it?). Provide the time indicated on the clock.



---

---

---

---



---

---













---

---



**Zoezi D**

Create four sentences using the time expressions and action verbs provided in each row below.

<b>Time visual</b>	<b>Shughuli A</b>	<b>Shughuli B</b>
1. 	 6:00	 8:30
2. 	 12:15	 2:45
3. 	 4:20	 5:33
4. 	 8:50	 9:45



## Zoezi E

One morning Joseph meets Shamila as she is leaving the library. Read their conversation and answer the questions that follow.

**Joseph:** Habari za asubuhi Shamila?

**Shamila:** Salama sana. Na wewe je?

**Joseph:** Mimi niko salama. Habari za masomo?

**Shamila:** Nzuri sana. Unatoka wapi?

**Joseph:** Ninatoka darasa la anthropolojia? Na wewe je?

**Shamila:** Mimi ninatoka maktabani kusoma. Unapenda masomo ya anthropolojia?

**Joseph:** Ndiyo, ninapenda masomo ya Anthropolojia kwa sababu mimi hujifunza utamaduni wa Afrika Mashariki. Unaenda wapi sasa?

**Shamila:** Ninaenda ofisini mwa Mwalimu Bakari. Nina miadi na yeye saa tano kamili asubuhi. Je, sasa ni saa ngapi?

**Joseph:** Ni saa tano kasoro dakika tano asubuhi.

**Shamila:** Sawa, tutaonana jioni.

**Joseph:** Haya, kwaheri.

**Shamila:** Kwaheri.

1. Miadi ya Shamila iko saa ngapi?
2. Joseph anatoka kwenye darasa gani?
3. Shamila anatoka wapi sasa?
4. Kwa nini Joseph anapenda masomo ya Anthropolojia?
5. Nyinyi huanza darasa la Kiswahili saa ngapi?
6. Nyinyi humaliza darasa la Kiswahili saa ngapi?



## Zoezi F

Pretend you are walking on campus one morning and you meet with one of your Kiswahili classmates. Exchange greetings to check on your friend. Ask your friend at least five questions about what they are currently doing and other plans they have for the day. Use the present tense with times that the activities are going to take place.





## Zoezi G

During one of the lessons in the study abroad program, Shamila and her Kiswahili teacher engage in a conversation about her daily routine. Read the conversation and answer the questions that follow.

**Mwalimu Bakari:** Hujambo Shamila?

**Shamila:** Sijambo Mwalimu na wewe je?

**Bakari:** Mimi sijambo. Habari za masomo?

**Shamila:** Salama kabisa, ila kazi ni nyingi.

**Bakari:** Pole. Je, wewe huamka saa ngapi?

**Shamila:** Mimi huamka saa kumi na mbili asubuhi.

**Bakari:** Baada ya kuamka, wewe hufanya nini?

**Shamila:** Mimi hutandika kitanda, hupiga mswaki, huoga, kisha hula chakula cha asubuhi na baadaye huenda chuoni.

**Bakari:** Baada ya darasa la Kiswahili wewe hufanya nini?

**Shamila:** Baada ya darasa mimi huenda maktabani kusoma vitabu na magazeti, kisha huenda kucheza mpira na rafiki zangu.

**Bakari:** Wewe hufanya nini wakati wa jioni baada ya shule?

**Shamila:** Mimi hufanya kazi ya nyumbani, humsaidia Bibi Farida kupika chakula cha jioni, hupiga pasi, huosha vyombo na hupanga nyumba. Kisha hulala saa nne usiku.

**Bakari:** Wewe huwa na shughuli nyingi sana kila siku.

**Shamila:** Bila shaka.

**Bakari:** Kwaheri. Tutaonana baadaye.

**Shamila:** Kwaheri. Siku njema.

1. Shamila hufanya nini baada ya kuamka asubuhi?
2. Baada ya darasa la Kiswahili Shamila hufanya nini?
3. Shamila hufanya nini katika maktaba?
4. Kabla ya kulala Shamila hufanya shughuli gani?
5. Shamila hulala saa ngapi?
6. Wewe hulala saa ngapi kila siku?



## Zoezi H

As part of their homework, Professor Bakari paired the students participating in the Kiswahili study abroad program so that they can exchange emails about how they spend a typical day. Joseph's partner Eray, his classmate from Turkey, sent an email yesterday asking Joseph about his weekly schedule. Read Joseph's reply below and answer the questions that follow.

Kwa Mpendwa Eray,

Hujambo rafiki. Habari gani? Habari za masomo? Familia hawajambo? Mimi sijambo. Ninapenda Tanzania sana. Eray, masomo ni mazuri lakini kazi ni nyingi sana. Kila siku mimi hulala mapema na pia huamka mapema. Kwa kawaida huamka saa kumi na moja kamili asubuhi. Kwanza, huoga, hujitayarisha na hula chakula cha asubuhi. Kutoka siku ya Jumatatu hadi Alhamisi huenda shuleni saa mbili asubuhi hadi saa kumi za jioni. Ijumaa mimi huwa chuoni hadi saa sita. Baada ya kurudi nyumbani hupiga gumzo na rafiki zangu na hucheza michezo, hula chakula cha jioni, hutazama televisheni na hulala saa tatu unusu usiku. Siku ya Jumamosi huenda sokoni kununua vyakula, hutembelea miji mbali mbali, huogelea na hupumzika sana. Siku ya Jumapili asubuhi, mimi huenda kanisani pamoja na familia yangu. Baadaye hufua nguo na husafisha nyumba. Kisha hupika chakula cha jioni, hufanya kazi ya nyumbani, na husoma ili kujiandaa kwa wiki mpya. Mimi hulala saa nne kamili usiku.

Asante na kwaheri.

Rafiki yako,

*Joseph*

1. Kwa kawaida, Joseph huamka saa ngapi?
2. Joseph hufanya nini kabla ya kwenda chuoni?
3. Joseph huenda shuleni siku gani za wiki?
4. Joseph hufanya nini siku ya Jumamosi?
5. Jumapili baada ya kutoka kanisani, Joseph hufanya nini?
6. Kwa nini Joseph husoma Jumapili usiku?
7. Fikiri wewe ni Eray, jibu barua pepe ya Joseph.



## Zoezi I

Assume your Kiswahili classmate sent you a direct message on Instagram asking what you do on a typical day. Write a few sentences and, where possible, include pictures in your response.



## Zoezi J

At the beginning of the study abroad program, all students were asked to keep a journal of their key daily activities. Present the regularly occurring activities that you would have in your journal to your classmates.

## Cultural Explorations

In East Africa, like other regions near the equator, there are an equal number of hours of daylight and night throughout the entire year. Sunrise is consistently around 7 a.m. and sunset is consistently around 7 p.m.; this is notably different from the U.S. and other Western countries where long days in the summer alternate with shorter days during the winter. This consistent period of daylight throughout the year makes it easy for East Africans to tell time reliably by the position of the sun or by looking at the length of shadows, much as ancient civilizations did using sundials. The day begins with long shadows extending to the west and those shadows get shorter until midday when the sun is overhead and there are little to no shadows; in the afternoon, the shadows lengthen toward the east until it gets dark.



Because the position of the sun and the shadows that it casts are so consistent, people in rural areas can get a general sense of the time from the world around them and there is no need to be focused on small (and largely meaningless) distinctions of time.

While there is a greater reliance on clock time in urban areas, especially in dealing with activities that operate on strict schedules, East Africans do not share the preoccupation with punctuality that characterizes some other cultures. It is common for East Africans to arrive later than an agreed upon time without explanation or apology. Similarly, arriving at someone's house at exactly the time specified may create an awkward situation as your host may be just beginning preparations for guests or may not yet be dressed for the event. If you are invited to visit an East African home, be clear when you are actually expected to arrive.

This is not to say that there are not East Africans who take great pride in their punctuality. Indeed, as they integrate further into the global economy, there is a growing perception that they may need to conform to Western and Asian norms of punctuality to successfully conduct business.

## Cultural Reflections

With a classmate or in a small group, discuss the cultural information you have just read by answering the questions that follow.

1. How do you tell the time and how often do you rely on the time of the day for your daily routine or activities?
2. How important is punctuality and staying on schedule to you? How important are these things in your society compared to societies in Eastern Africa?
3. Would your day-to-day be different if you followed the customs related to time in East Africa?



## Zoezi K

Below is a brief description of how Farida and Juma spend a typical day. Read the description and answer the questions that follow.

Familia ya Bibi Farida na Bwana Juma wanaishi katika kijiji cha Iringa katika nchi ya Tanzania. Bwana Juma ni mkulima na Bibi Farida ni mhasibu. Kila siku wao huenda kazini na pia hufanya shughuli za nyumbani. Kuanzia siku ya Jumatatu hadi Ijumaa, wao huamka saa kumi na mbili asubuhi, Bibi Farida hupika chakula cha asubuhi na hupiga nguo pasi. Kisha, wao huoga, hupiga mswaki na huvaa nguo. Baadaye, wao hula chakula cha asubuhi na kisha wao huwapeleka watoto shuleni na huenda kazini. Bwana Juma huenda shambani kulima. Bibi Farida huenda ofisini kufanya kazi. Wao hurudi nyumbani saa kumi na moja za jioni. Bibi Farida hupika chakula cha jioni na wao hula saa moja kamili. Baada ya kula chakula cha jioni, wao huwasaidia watoto wao na kazi za nyumbani, na hutazama televisheni pamoja na watoto wao kuanzia saa mbili hadi saa tatu kamili za usiku. Baadaye, wao hupiga mswaki, huoga na kila mtu hulala saa nne kamili. Wikendi, wao hufanya shughuli mbalimbali. Siku ya, Jumamosi, wao huamka saa mbili kamili, kisha wao hula chakula cha asubuhi na hufanya kazi shambani hadi saa sita mchana. Wao huenda sokoni jioni. Kisha, wao hupika chakula cha jioni, hula, huosha vyombo, na hulala saa tatu usiku. Siku ya, Jumapili, wao huenda kanisani saa moja kamili asubuhi. Baada ya kanisa wao hutembelea majirani wao kisha, huandaa watoto kwa wiki mpya.

1. Bibi Farida na Bwana Juma hufanya kazi gani?
2. Wao huamka saa ngapi kuanzia siku ya Jumatatu hadi siku ya Ijumaa?
3. Bibi Farida hufanya nini asubuhi baada ya kuamka?
4. Baada ya kuwapeleka watoto shuleni, Bwana Juma hufanya nini?
5. Ni nani huwasaidia watoto na kazi za nyumbani?
6. Siku ya Jumapili baada ya kuwatembelea majirani wao Bibi Farida na Bwana Juma hufanya nini?
7. Kuna tofauti gani kati ya ratiba yako na ya familia ya Farida na Juma kwenye wiki na katika wikendi?



## Zoezi L

You are trying to find a new roommate and want to be sure you have similar schedules. Exchange information with a few classmates to get to know their schedules so you can choose an appropriate roommate. Include details about specific days and times of the day.



### Zoezi M

Listen to Mwalimu Bakari describe his daily schedule in class. Then, fill in the graphic organizer below identifying the similarities and differences between your daily schedule and that of Mwalimu Bakari.

Mwalimu Bakari	Mimi	Mwalimu Bakari na mimi



### Zoezi N

Create a photo collage that shows your daily schedule for seven days. Make sure to include the section of the day and the different times you do these activities. Present your collage to your classmates.



### Zoezi O

Mwalimu Bakari divided the Kiswahili students into 3 groups and each group was asked to discuss their daily routines and then report back to the class. Read Joseph's report below and answer the questions that follow.

Kila siku asubuhi, mimi huamka, hula chakula cha asubuhi kisha huenda shuleni. Anita huamka asubuhi, kisha yeye husoma na baadaye huenda shuleni. Lakini Eray hufanya mazoezi kila siku asubuhi baada ya kuamka, kisha yeye huoga na kula chakula cha asubuhi. Mimi sipendi kufanya mazoezi asubuhi kama Eray kwa sababu, mimi huenda shuleni kwa baiskeli kila siku. Kila siku jioni, Eray na Anita huogelea kisha wao huenda maktabani lakini mimi huenda kucheza mpira. Sisi wote hutazama televisheni jioni kisha huoga na hulala.

*Is it true (kweli) or false (si kweli)? If false, make the necessary changes to create a true statement.*

1. Joseph, Eray na Anita huenda shuleni kabla ya kula chakula cha asubuhi.
2. Anita na Eray huogelea kila siku asubuhi kabla ya kuhudhuria vipindi vya masomo.
3. Joseph hupenda kucheza soka lakini hapendi kuogelea.

4. Anita husoma asubuhi lakini jioni hupenda kutazama televisheni.
5. Eray, Anita na Joseph hulala kabla ya kuoga.
6. Joseph hufanya mazoezi kila asubuhi.



### Zoezi P

Interview two classmates about their daily schedules. Ask at least five questions. Be prepared to report your findings to the other students in class.



### Zoezi Q

While on a visit to Tanzania, you decide to go hiking on the weekend. You happen to meet one of your classmates who is also looking for a hiking partner. Exchange information about the activities you usually engage in at different times of the day to see if you can find a time to go hiking together.

### Sarufi: Kukanusha hali ya mazoea (*Negation of the habitual tense*)

To negate the habitual tense, one uses the negated present tense form and places the word *huwa* in front of that verb.

Mimi **huenda** kazini saa mbili asubuhi.  
Mimi **huwa siendi** kazini saa mbili asubuhi.

*I go to work at 8am.*  
*I do not go to work at 8am.*

Wao **hupenda** kucheza kandanda.  
Wao **huwa hawapendi** kucheza kandanda.

*They like playing soccer.*  
*They do not like playing soccer.*

Mimi **huishi** katika mji wa Nairobi.  
Mimi **huwa siishi** katika mji wa Nairobi.

*I live in Nairobi city.*  
*I do not live in Nairobi city.*



### Zoezi R

Interview at least two classmates about their typical daily schedule. Make sure to ask what they do at specific times of the day. After the interviews, be prepared to share what you learned.



## Zoezi S

Listen as Shamila describes her daily schedule to her classmates and answer the questions that follow.

Hamjambo? Jina langu ni Shamila. Mimi ni mwanafunzi wa Kiswahili hapa Chuoni Dar es Salaam na mimi huenda shuleni kila siku. Kila siku, mimi huwa na shughuli mbalimbali shuleni na nyumbani. Kwa kawaida mimi huamka saa moja asubuhi kila siku, kisha mimi hupiga mswaki, huoga na huenda darasani. Mimi huwa sipendi kula chakula cha asubuhi kwa sababu sina muda wa kutosha na mimi hula polepole. Baada ya darasa la Kiswahili, mimi hula chakula cha mchana na kisha huenda maktabani. Mimi sipendi kusomea darasani kwa sababu kuna kelele sana. Baada ya kusoma mimi na rafiki yangu huenda kucheza mpira wa vikapu. Baadaye mimi huenda nyumbani, hupika chakula cha jioni, hula, hupumzika na husoma kidogo. Huwa sipendi kutazama televisheni wakati wa jioni kwa sababu huwa nimechoka sana. Baada ya kumaliza kazi ya nyumbani, mimi hulala saa nne usiku. Mimi huwa sipendi kulala baada ya saa nne za usiku kwa sababu huenda shuleni mapema.

*Is it true (kweli) or false (si kweli)? If false, make the necessary changes to create a true statement.*

1. Shamila ni mwanafunzi katika chuo kikuu cha Dodoma.
2. Shamila anapenda kula chakula cha asubuhi.
3. Shamila hula chakula cha mchana kabla ya darasa la Kiswahili.
4. Shamila anapenda kusoma darasani.
5. Shamila hucheza mpira wa vikapu pamoja na rafiki yake.
6. Shamila anapenda kutazama televisheni.
7. Shamila hulala kabla ya saa nne usiku kila siku.
8. Shamila huenda shuleni mapema.

## Key Vocabulary

### *Adjectives*

<b>bora</b>	better; suitable
<b>-fupi</b>	short; brief
<b>kamili</b>	complete; exact
<b>muhimu</b>	important
<b>-pya</b>	new; recent; modern
<b>-refu</b>	tall; long

### *Nouns*

<b>alasiri</b>	late afternoon; early evening
<b>alfajiri</b>	dawn; daybreak
<b>asubuhi</b>	morning
<b>baiskeli</b>	bicycle
<b>dakika</b>	minute
<b>jioni</b>	evening
<b>kelele</b>	noise
<b>kitabu</b>	book
<b>maisha</b>	life
<b>mchana</b>	afternoon
<b>meza ya lugha ya Kiswahili</b>	Kiswahili table ( <i>a get together for practicing Kiswahili</i> )
<b>miadi</b>	appointment
<b>mpira wa vikapu</b>	basketball
<b>mtaa</b>	neighborhood; street; suburb
<b>muda</b>	time; period of time
<b>nusu</b>	half
<b>saa</b>	hour; o'clock
<b>sekunde</b>	second ( <i>measurement of time</i> )
<b>shamba</b>	farm
<b>usiku</b>	night; nighttime
<b>utafiti</b>	research
<b>vitu vingi</b>	many things
<b>wikendi</b>	weekend

### *Verbs*

<b>-andaa</b>	to provide; to prepare
<b>-anza</b>	to start
<b>-choka</b>	to be tired; to feel tired
<b>-fanya kazi (ya) shambani</b>	to work in the field; to do farm work
<b>-fanya utafiti</b>	to do research
<b>-fika</b>	to arrive
<b>-furahia</b>	to feel extremely happy; to be joyful
<b>-kamilisha</b>	to complete
<b>-kutana</b>	to meet
<b>-lima</b>	to farm
<b>-maliza</b>	to end; to finish
<b>-ondoka</b>	to leave
<b>-peleka</b>	to send
<b>-rudi</b>	to return



**-tandika kitanda** to make the bed  
**-uliza** to ask; to inquire

## Key Phrases


**Haya!** Ok! That's that!  
**huanza saa...** I start at...  
**hufika saa...** I arrive at...  
**humaliza saa...** I finish at...  
**huondoka saa...** I leave/depart at...  
**hurudi...** I return...  
**huwa siendi...** I do not go...  
**...ili niweze...** ...so that I can...  
**kasorobo** a quarter to  
**kati ya (6:00) na (7:00)** between (6:00) and (7:00)  
**kutoka (Jumatatu) hadi (Ijumaa)** from (Monday) to (Friday)  
**kutoka saa (6:00) hadi saa (7:00)** from (6:00) until (7:00)  
**kwa muda wa...** for the duration of...  
**...kwa siku; ...kwa wiki** ...per day; ...per week  
**mimi hukamilisha...** I complete...  
**Ni saa...** It is... o'clock.  
**robo** a quarter after/past  
**saa (mbili) kamili** 8 o'clock exactly/sharp  
**saa (mbili) kasorobo** a quarter to (8 o'clock)  
**saa (mbili) na nusu** half past 8 o'clock  
**saa (mbili) na robo** a quarter after/past 8 o'clock  
**(Sasa) ni saa ngapi?** What time is it (now)?  
**Sawasawa!** Right! Okay!

### 3.4 Shughuli za starehe



#### Zoezi A

Mwalimu Bakari and his family went on vacation for a week, as they do every year. Upon returning, he shared with his students his vacation schedule. Read his descriptions and fill in the table below to indicate what activities Mwalimu Bakari and his family did on each of the days.



Wiki iliyopita nilikuwa na shughuli nyingi sana. Mimi na familia yangu tulisafiri kwenda mjini Arusha kutoka siku ya Jumatatu hadi siku ya Jumamosi. Tulianza safari siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. Tulifika Arusha saa nane za mchana. Baada ya kufika, tulikula chakula cha mchana, kisha tulienda kumtembelea rafiki yangu Bwana Sudi. Siku ya Jumanne, tulienda kwenye maktaba pamoja na watoto wangu kusikiliza hadithi za watoto kutoka saa nne za asubuhi hadi saa sita za mchana. Kisha, tulienda sokoni kununua vyakula na matunda tofauti tofauti. Saa za jioni tulipika vyakula, kisha tulicheza michezo ya bodi na kadi. Siku ya Jumatano tulihudhuria sherehe za kitamaduni mjini Arusha kutoka asubuhi hadi alasiri. Wakati tulipofika nyumbani tulikuwa tumechoka sana, kwa hivyo hatukufanya kazi yoyote. Tulilala saa mbili za usiku. Siku ya Alhamisi, mimi na mke wangu tulienda kutazama sinema, na watoto wetu walienda kutembelea shangazi yao anayeishi karibu na mlima wa Arumeru, kilomita chache kutoka mji wa Arusha. Walipokuwa kwa shangazi yao, walimsaidia kuvana mahindi na kuyapanga kwenye ghala. Siku ya Ijumaa, tulipumzika asubuhi, kisha tulienda kusali msikitini wakati wa alasiri. Baada ya kutoka msikitini tulienda ufukweni kuogelea, kubarizi na kupiga gumzo. Watoto walicheza michezo mbali mbali. Jumamosi tulirejea nyumbani. Tulifurahia likizo yetu sana.

<b>Siku ya Jumatatu</b>	
<b>Siku ya Jumanne</b>	
<b>Siku ya Jumatano</b>	
<b>Siku ya Alhamisi</b>	
<b>Siku ya Ijumaa</b>	
<b>Siku ya Jumamosi</b>	



### Zoezi B

Assume you went for a week long vacation to your favorite destination. Your classmates would like to know the various daily activities you engaged in during the vacation. Role play the conversation with two classmates.

### Msamiati: -penda (*like metric*)

Similar to the way English speakers use the verb *to like* when talking about their hobbies, Kiswahili speakers use the verb *-penda* to denote what they like or love doing. There are, however, several levels of liking something, which can be referred to as a like metric. Below is a chart that indicates a like metric from least to most in Kiswahili.

**LEAST**

**MOST**

sipendi	sipendi sana	ninapenda kiasi	ninapenda kidogo	ninapenda	ninapenda sana	ninapenda zaidi
---------	--------------	-----------------	------------------	-----------	----------------	-----------------



## Zoezi C

One weekend Shamila calls her friend, Alisa, who is studying in Kenya, so that they can catch up. Alisa would like to know what Shamila has been doing for fun. Read their conversation and prepare the activity that follows.



**Shamila:** Hujambo Alisa. Habari za siku nyingi?

**Alisa:** Nzuri sana. Habari za masomo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam?

**Shamila:** Salama sana. Ninapenda sana masomo hapa kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Na wewe habari za kazi?

**Alisa:** Nzuri sana ila nina kazi nyingi sana.

**Shamila:** Pole kwa kazi.

**Alisa:** Asante. Wewe unapenda kufanya nini wakati wa kupumzika?

**Shamila:** Kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, mimi huwa na shughuli nyingi sana. Kwa hivyo, mimi hupumzika wikendi. Ninapenda wikendi zaidi ya siku zingine zote za wiki.

**Alisa:** Wewe hupenda kufanya nini Jumamosi?

**Shamila:** Kwa kawaida, mimi husikiliza muziki wa Bongo na hutazama vipindi katika televisheni wakati wa mchana. Ninapenda zaidi muziki wa Bongo kuliko kusikiliza muziki wa Reggae. Mimi sipendi kuogelea sana hapa Dar es Salaam.

**Alisa:** Je, wewe huenda kwenye sinema?

**Shamila:** Ndiyo, mimi ninapenda sana kwenda kwenye sinema. Mimi na rafiki zangu huenda sinema kila Jumamosi jioni.

**Alisa:** Vizuri sana. Nimefurahi kuzungumza na wewe leo. Tutazungumza tena wikendi ijayo.

**Shamila:** Sawa. Asante sana rafiki.

**Alisa:** Kwaheri!

**Shamila:** Kwaheri na wakati mwema!

**Alisa:** Nakutakia wakati mwema pia!

Discuss the questions below with a classmate. Be prepared to present your responses to the rest of the class.

1. Je, Shamila anapenda masomo yake huko Dar es Salaam? Je, unapenda kusoma Kiswahili? Je, rafiki yako anapenda kusoma masomo gani? Kwa nini unapenda/hupendi kusoma Kiswahili?
2. Ni siku gani Shamila huwa na shughuli nyingi sana? Je, yeye anapenda siku gani zaidi na kwa nini anapenda siku hizi? Wewe na rafiki yako mnapenda siku za wikendi au siku gani za wiki? Kwa nini mnazipenda siku hizi?
3. Shamila na rafiki zake huenda sinema siku gani? Unapenda kwenda sinema wikendi? Kati ya wewe na rafiki yako ni nani anapenda kwenda kwenye sinema zaidi? Unafikiri watu wengi Afrika Mashariki au Tanzania huenda kwenye sinema?
4. Je, Shamila anapenda kuogelea kila siku? Wewe na rafiki yako mnapenda kuogelea? Kati yako na rafiki yako, ni nani anapenda kuogelea zaidi? Watu wengi katika jamii yako hupenda au hawapendi kuogelea?

### **Sarufi: Wakati uliopita (*Past tense*)**

So far, you have been introduced to the present and habitual tenses and how to create negated forms of each. These are both helpful if you want to talk about actions that are currently taking place or that take place on a regular basis.

In this unit, you will focus on the past tense, which can be identified by the use of the marker *-li-* used exactly as we used the marker *-na-* to indicate the use of the present tense.

Ninaishi Kenya

*I live in Kenya.*

Niliishi Kenya nikiwa mtoto.

*I lived in Kenya as a child.*

Ninasoma Kiswahili.

*I am studying Kiswahili.*

Nilisoma Kiswahili katika chuo kikuu.

*I studied Kiswahili in college.*

You will also see a form of the past tense used to describe a sequence of actions that happened in the past. This is usually called the **narrative tense** and can be identified by the use of the marker *-ka-*. There is not a direct English equivalent for this tense, but the *-ka-* marker usually follows a *-li-* marker if there are a string of consecutive actions.

Mimi niliamka asubuhi, nikaoga, nikapika kisha nikaenda shuleni.

*I got up in the morning, showered, made some food, and then went to school.*



## Zoezi C

On Monday morning, Shamila and Joseph talk about what they did over the weekend. Read their conversation and answer the questions that follow.

**Shamila:** Habari za asubuhi Joseph.

**Joseph:** Nzuri sana. Wikendi yako ilikuwaje?

**Shamila:** Wikendi ilikuwa nzuri sana.

**Joseph:** Ulifanya nini wikendi?

**Shamila:** Mimi na familia yangu tulisafiri hadi Kilimanjaro. Na wewe ulifanya nini wikendi?

**Joseph:** Siku ya Jumamosi, mimi nilienda kutazama filamu ya *Bahasha* na rafiki zangu. Jumapili familia yangu pokezi na mimi tulifanya shughuli za usafi na pia tuliwapokea wageni.

**Shamila:** Uliipenda filamu?

**Joseph:** Ndiyo, niliipenda sana.

**Shamila:** Je, wageni wenu walisafiri kutoka wapi?

**Joseph:** Wageni hao walisafiri kutoka Morogoro. Nilifanya mazoezi ya mazungumzo ya Kiswahili nao. Waliondoka Jumapili mchana.

**Shamila:** Vizuri sana. Sisi tulisafiri hadi Kilimanjaro Ijumaa na tulirejea Jumapili.

**Joseph:** Mlifanya nini kule Kilimanjaro?

**Shamila:** Tulikwea mlima, tukatazama mandhari, tukasoma kuhusu historia ya hifadhi ya Kilimanjaro na tukapiga picha juu ya mlima.

1. Shamila alisafiri kwenda wapi wikendi iliyopita?
2. Joseph alifanya nini siku ya Jumamosi?
3. Wageni ambao walitembelea familia pokezi ya Joseph walisafiri kutoka wapi?
4. Wageni wa familia ya Joseph waliondoka lini?
5. Shamila na familia yake walifanya nini katika ziara yao ya Kilimanjaro?



## Zoezi D

In the past week, you were not able to attend your Kiswahili class three days in a row due to an important event that you had to attend. You meet with your teacher after class to let him or her know why you were absent from class. With a classmate, roleplay this conversation twice so that each of you can practice as the teacher and as the student.



### Zoezi E

Using the model of Mwalimu Bakari’s travel schedule at the start of this unit, describe the activities you did during your free time last week, making sure to include the specific times and days that you did them. You will present your schedule to your classmates.



### Zoezi F

When talking about events that happened in the past, Kiswahili speakers might use *jana* (yesterday) and *juzi* (day before yesterday) rather than referring to the day of the week. Use these words to form five questions to ask your classmates about their daily activities.

#### **Examples:**

Jana asubuhi ulifanya nini baada ya kuamka?  
Juzi jioni baada ya shule ulifanya nini?



### Zoezi G

Using the questions you created in *Zoezi F*, interview two classmates about what they did for fun over the weekend. Then, create a report that you will present in class.



### Zoezi H

Create a collage of your favorite celebrity to highlight their most recent vacation, especially the leisure activities they did. Present your collage to your classmates.



### Zoezi I

Over the weekend, one group of students went to Mount Kilimanjaro while another group went camping at Serengeti National Park. Pick the group that you were in and then find a classmate who went on the other trip. Have a conversation about the activities you did on your trips.



### Zoezi J

Baraka recorded a description of what he typically does during the weekend. Listen to the recording and answer the questions that follow.

1. Kwa nini Baraka hupumzika wikendi?
2. Yeye hufanya nini baada ya kuamka Jumamosi asubuhi?
3. Kwa nini Baraka husoma gazeti la spoti Jumamosi?
4. Kabla ya kulala Baraka hufanya nini siku ya Jumamosi?
5. Baraka na familia yake hufanya nini Jumapili baada ya kanisa?





## Zoezi K

Mwalimu Bakari showed his class the pictures below, which depict daily activities that his family does regularly. Do you do similar activities regularly? Why or why not? Discuss your answers with a classmate.



kucheza kandanda



kuogelea



kucheza densi



kukimbia



kuosha vyombo



kulima



kukama ng'ombe



kucheza voliboli



kulisha ng'ombe



## Zoezi L

Prepare a blog post about your daily activities during a hypothetical study abroad trip to Tanzania. Include a few memorable pictures so that you can share them with your host family, friends, and the wider Kiswahili-speaking community.



## Sarufi: Kukanusha wakati uliopita (*Negating past tense*)

When expressing an action that did *not* take place in the past, the marker *-ku-* is used with the negated subject markers (e.g., *si*, *hatu*, *hawa*, etc.) and the root of the verb.

Ni <b>li</b> tembea mjini Dar es Salaam.	<i>I walked around Dar es Salaam.</i>
Si <b>ku</b> tembea mjini Dar es Salaam.	<i>I did not walk around Dar es Salaam.</i>
Tu <b>li</b> kula chakula cha Afrika Mashariki.	<i>We ate East African food.</i>
Hatu <b>ku</b> kula chakula cha Afrika Mashariki.	<i>We did not eat East African food.</i>
U <b>li</b> safisha nyumba.	<i>You cleaned the house.</i>
Hu <b>ku</b> safisha nyumba.	<i>You did not clean the house.</i>
Ali <b>and</b> ika barua pepe.	<i>He/she wrote an email.</i>
Haku <b>and</b> ika barua pepe.	<i>He/she did not write an email.</i>



### Zoezi M

Shamila and Joseph talk about their weekend when they meet on Monday morning. Read their conversation and answer the questions that follow.

**Shamila:** Vipi Joseph? Habari za wikendi?

**Joseph:** Nzuri tu. Wikendi ilikuwa safi kabisa. Mimi na rafiki zangu tulienda kutembea kwenye mji wa Morogoro. Je, wewe ulienda na wanafunzi wengine kukwea mlima Kilimanjaro?

**Shamila:** Hapana, mimi sikuenda kukwea mlima Kilimanjaro, nilienda na mama katika Kisiwa cha Unguja.

**Joseph:** Safi kabisa. Mliondoka lini?

**Shamila:** Tuliondoka Ijumaa asubuhi.

**Joseph:** Je, mlirudi Jumapili?

**Shamila:** Hapana hatukurudi Jumapili. Tulirudi Jumatatu jioni.

**Joseph:** Sawa. Tutaongea mengi baadaye.

1. Shamila alisafiri kwenda wapi wikendi?
2. Je, Shamila alisafiri peke yake?
3. Shamila aliondoka siku gani kwenda kwenye safari?
4. Shamila walirudi nyumbani siku gani?
5. Je, Joseph na rafiki zake walienda kukwea mlima Kilimanjaro?
6. Joseph na rafiki zake walirudi lini?



### Zoezi N

Poll two classmates to find out what activities they did this past weekend. Be prepared to report back to the class.



### Zoezi O

In pairs, interview a classmate about their favorite vacation. Some helpful interview questions are provided in the list below. Be prepared to report the details you gather to the class.

***Examples:***

- Ulienda wapi?
- Ulienda na nani?
- Ulifanya nini?
- Ulipenda nini zaidi?
- Hukupenda kitu gani?

## Key Vocabulary

### Nouns

<b>alasiri</b>	late afternoon
<b>chumba</b>	room
<b>gazeti la spoti</b>	sports magazine
<b>ghala</b>	storage
<b>hifadhi ya Kilimanjaro</b>	Kilimanjaro Reserve
<b>kilomita</b>	kilometer
<b>kipindi (vipindi)</b>	program (programs)
<b>kisiwa</b>	island
<b>kitabu cha hadithi (ya Kiswahili)</b>	Kiswahili storybook
<b>likizo</b>	vacation
<b>mahindi</b>	maize; corn
<b>mazoezi ya mazungumzo</b>	speaking exercises; conversation practice
<b>mchezo wa karata</b>	card game
<b>mchezo wa bodi</b>	board game
<b>mlima</b>	mount; mountain
<b>mpira wa kandanda</b>	soccer ball
<b>picha</b>	picture
<b>ratiba</b>	schedule; itinerary
<b>safari</b>	a trip
<b>shamba</b>	farm
<b>sherehe (ya kitamaduni)</b>	(cultural) celebration
<b>shughuli za usafi</b>	cleaning tasks; chores
<b>sinema</b>	cinema; movie theater
<b>voliboli</b>	volleyball
<b>wikendi ijayo</b>	next weekend

### Verbs

<b>-barizi</b>	to chill; relax
<b>-cheza densi</b>	to dance
<b>-cheza kandanda</b>	to play football (soccer)
<b>-choka</b>	to be tired; to be exhausted
<b>-kama (ng'ombe)</b>	to milk (cows)
<b>-kua</b>	to grow; to grow up
<b>-kwea</b>	to climb; to ascend
<b>-lima</b>	to farm; to plow
<b>-lisha (ng'ombe)</b>	to feed (cows)
<b>-ondoka</b>	to leave; to depart
<b>-penda</b>	to like
<b>-penda kidogo</b>	to like a little bit
<b>-penda sana</b>	to like very much
<b>-penda zaidi</b>	to like greatly
<b>-piga</b>	to beat; to hit
<b>-piga gumzo</b>	to chat
Hii ni **sebule** katika nyumba ya wazazi wangu. Kuna vitu vingi katika sebule. Kuna kochi moja ambalo lina mito miwili midogo. Katikati ya sebule kuna meza moja ndogo. Meza hiyo iko juu ya zulia. Pia kuna viti viwili. Katikati ya viti viwili kuna meza ambayo ina mmea. Kuna taa mbili. Taa moja inaning'inia katikati ya paa na nyingine iko katika kona karibu na kabati dogo. Kuna dirisha moja kubwa ambalo lina pazia jeupe. Picha mbalimbali zimetundikwa kwenye ukuta.



Hiki ni **chumba changu cha kulala**. Chumba hiki si kikubwa sana. Katika chumba kuna kitanda kikubwa ambacho kina godoro, shuka, na mito. Kando ya kitanda kuna makabati mawili madogo ambayo yana taa na vitu vingine vidogo vidogo kama vile saa, karatasi, shashi na kadhalika. Kwenye ukuta nimetundika picha ya sanaa ambayo ninaipenda mno. Chumba hiki kina madirisha mawili makubwa ambayo yana pazia kubwa.



Hii hapa ni **jikoni** yetu. Katika jikoni kuna jiko, friji, mashine ya kuosha vyombo, jaa la takataka na sinki. Kuna makabati ya chini na makabati ya juu. Kuna aina mbalimbali za vyombo katika makabati haya. Mama yangu anapenda kupika, kwa hivyo yeye huweka vyombo kama vile sahani, vikombe, vijiko, mabakuli na glasi katika makabati ya juu. Na makabati ya chini hutumiwa kuweka sufuria, vikaango, vijiko na visu. Sisi huweka vyakula mbalimbali katika kabati pia.



**Chumba cha maakuli** chetu kina vitu mbalimbali. Kuna meza kubwa na viti vinne. Kando ya meza na viti kuna kabati ambalo lina vyombo mbalimbali vya kulia kama vile sahani, birika, uma, visu na vijiko. Juu ya kabati hili kuna ua.

1. Je, sebule katika nyumba hii ina vitu gani?
2. Makabati katika jikoni yanatumiwa kuweka vitu gani?
3. Kwenye kuta za nyumba hii kuna vitu gani?
4. Kando ya kitanda katika chumba cha kulala cha Joseph kuna vitu gani?
5. Je, sakafu ya chumba cha maakuli ina zulia?
6. Kuna viti vingapi katika chumba cha maakuli?
7. Kuna vitu gani katika sebule, jikoni, chumba chako cha kulala, na chumba cha maakuli?



### Zoezi D

The class will work as a group to describe an imaginary room with each person adding a new object. The first person will name an object in the room (*Katika sebule kuna kochi*). The next person will repeat that object and then add one of their own (*Katika sebule kuna kochi na televisheni*). Each successive person must repeat all of the objects mentioned before adding their own. See how many objects you can remember!



### Zoezi E

Listen to Shamila's description of her home back in Kansas and answer the following questions.

1. Shamila huweka vitu gani katika kabati dogo ambalo liko msalani mwa chumba chake?
2. Misala mingine iko katika vyumba gani kwenye nyumba ya familia ya Shamila?
3. Kuna vitu gani vingine msalani katika chumba cha Shamila?
4. Banda la gari la nyumba ya familia ya Shamila linatoshea magari mangapi?
5. Shamila na familia yake huweka vitu gani vingine katika banda lao la gari?



### Zoezi F

Compare Joseph's descriptions of his home in California in *Zoezi C* above with at least two rooms in your own house. Share with the class the similarities and differences that you note.



### Zoezi G

Listen to the description Joseph's friend from Kenya gives for his new apartment in the United States and answer the following questions.

1. Abdi anakaa katika jimbo gani?
2. Je, Abdi anakaa katika apatmenti pekee yake?
3. Katika mji wa Tallahassee kuna taasisi gani za masomo?
4. Apatmenti ya Abdi ina vyumba gani?
5. Nyumba ya Abdi ina vitu gani katika sebule, chumba cha kulala, na jikoni?



### Zoezi H

A friend from your hometown will attend the same college as you next fall and needs to find a place to live. Your friend would like to know more about where you live and whether or not they could be your roommate. Role-play this conversation with a classmate.



### Zoezi I

Imagine that you will be travelling to Dar es Salaam with your classmates over the next break. Work in pairs to find suitable housing via a website like Airbnb. You can rent an apartment or join together with another group to rent a larger house. Be prepared to show and to describe the accommodations as well as to explain why you chose them.



### Zoezi J

Write a detailed description of your dream house. Where is it located? What kind of house is it? How many rooms does the house have? What things does each room have? Be prepared to present the description to the class.



### Zoezi K

Take turns presenting your description of your dream house to the class. After everyone has presented, the class will vote for their favorite house.

## Sarufi: Ngeli ya N-N (*N-N Noun Class*)

The *N-N* noun class is the broadest class, and nouns from this class include manufactured products, places, abstract concepts, foods, and most words of foreign origin. As there are so many foreign borrowings in this class, most nouns in this class do not, in fact, start with the prefix *n-*. Nouns in this class have identical prefixes in the singular and plural forms.

nyumba – *house; houses*  
sahani – *plate; plates*

sufuria – *pot; pots*  
picha – *picture; pictures*

For verbal prefixes, this noun class uses *i-* in singular and *zi-* in plural for sentence formation.

Ndege **i**meondoka.  
Ndege **zi**meondoka.

*The plane has departed.*  
*The planes have departed.*

Hospitali **i**lifungwa.  
Hospitali **zi**lifungwa.

*The hospital was closed.*  
*The hospitals were closed.*

Picha **i**tatundikwa ukutani.  
Picha **zi**tatundikwa ukutani.

*The picture will be hung on the wall.*  
*The pictures will be hung on the wall.*

Sahani **i**ko juu ya meza.  
Sahani **zi**ko juu ya meza.

*The plate is on the table.*  
*The plates are on the table.*

Kompyuta **i**ko katika chumba cha kulala.  
Kompyuta **zi**ko katika chumba cha kulala.

*The computer is in the bedroom.*  
*The computers are in the bedroom.*

Kompyuta **i**meanguka chini kutoka mezani.  
Kompyuta **zi**meanguka chini kutoka mezani.

*The computer has fallen off the table.*  
*The computers have fallen off the table.*



## Zoezi L

Write the following sentences in the plural form.

1. Sahani iko karibu na sinki.

---

2. Friji yake imeharibika.

---

3. Benchi ya kupumzika imeanguka.

---

4. Sanamu iko karibu na televisheni.

---

5. Glasi ya kunywa maji imevunjika.

---

6. Jaa la takataka liko katika kila chumba nyumbani.

---

7. Kompyuta yangu imechafuka.

---

8. Nyumba imeoshwa.

---

9. Taulo yake iko nje.

---

10. Chai imepikwa.

---



## Zoezi M

Use the words or phrases provided below to complete the sentences. Use each word or phrase only once.

**kitanda | kina | kuna | maakuli | ambayo | ambacho  
meza | bafu | kulala | nina | karibu na | kubwa**

1. Ningependa kununua nyumba \_\_\_\_\_ ina vyumba vingi kwa kuwa \_\_\_\_\_ familia kubwa.
2. Kila chumba \_\_\_\_\_ kiko kwenye nyumba ya Bwana Kizito. \_\_\_\_\_ choo na bafu.
3. Kuna \_\_\_\_\_ kubwa ambalo liko karibu na sebule.
4. Katika nyumba hii \_\_\_\_\_ kioo kikubwa ambacho kiko kwenye \_\_\_\_\_ na pia kwenye choo.
5. Kwenye kila chumba cha \_\_\_\_\_ kuna \_\_\_\_\_.
6. Bwana Bakari angependa kununua nyumba \_\_\_\_\_ Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
7. Bwana Bakari anataka nyumba \_\_\_\_\_ yenye vyumba sita.



## Zoezi N

Baraka had a break-in at his home, and several things were stolen. Listen carefully to his voicemail to hear what was taken. Then, answer the questions that follow in complete sentences, giving as many details as you can.

1. Kwa nini Baraka hawezi kwenda shuleni?

---

2. Wezi waliiba katika nyumba ya Baraka saa ngapi?

---

3. Je, Baraka alikuwa nyumbani wezi walipoingia?

---

4. Wezi waliiba vitu gani katika chumba cha kulala?

---

5. Katika chumba cha maakuli Baraka alipoteza vitu gani?

---

6. Baraka anahitaji kupiga ripoti wapi kuhusu tukio la wizi la nyumbani kwake?

---





### Zoezi O

Listen to the descriptions of Amina’s house that she is preparing to rent out. Then, complete the graphic organizer below, listing the items that are in each room.

<b>sebule</b>	<b>chumba cha kulala</b>	<b>jikoni</b>



### Zoezi P

Write an email to Amina describing items that she might want to buy for her house to make it more appealing to prospective renters.

## Cultural Explorations

The interior of houses (including the layout of rooms, furniture, and appliances) varies widely throughout East Africa. Like the housing itself, one will find a mix of traditional design and designs with varying degrees of Western influence, while the latter is more common in urban and suburban areas. New construction in more affluent rural areas also reflects a greater adherence to (sub)urban norms.

As a general rule, the amount of space in a house or apartment is likely to be less in East Africa than in Western countries. There is also a general conception that one does not have private space of their own. Siblings normally share a room while growing up, with many even sharing a bed. This feeling of communal life is further strengthened by a kitchen or bathroom shared among households living on a homestead.

Floors will typically be of hard surfaces (e.g., tile, mud, wood, or concrete) with rugs placed strategically for both comfort and aesthetics; you will not see wall-to-wall carpet typical of American homes. Furniture within the home will vary by the wealth of the occupants and the options readily available for purchase, but you would expect to find furniture similar to that in most Western homes. Clothes are generally stored within a built-in wardrobe or in storage containers rather than in a dresser or a closet.

Interior decoration is largely dependent on what is available locally. Urban homes are likely to include more manufactured and imported goods, whereas rural homes are more likely to showcase local crafts (e.g., woven floor mats, baskets, etc.). Although there will be some variation based on religious or cultural values and socioeconomic status, family pictures, calendars, posters and African art are also common in making a house more of a home.

Thanks to large government electrification projects, the number of people with access to electricity is growing at a very fast pace. As of 2019, about 70% of Kenyans and about 38% of Tanzanians had access to electricity in their homes. However, the urban/rural divide in this access is marked, with Kenya having 90.8% of the population with access in urban areas but 61.7% within rural areas and with Tanzania having 73.2% with access in urban areas but only 19% within rural areas.




Figure 1. Access to electricity (% of population) for Tanzania, Kenya (World Bank)

The main use of electricity within homes, at this point, is lighting. Cooking is done primarily by use of wood or coal, although propane and electric stoves are common in more urban settings. In low-income families that cannot afford a refrigerator, perishable food is bought as it is needed and consumed quickly.

### Cultural Reflections:

With a classmate or in a small group, discuss the cultural information you have just read by answering the questions below.

1. Community and communal living are an important aspect for East African families. Is this an expected way of living in your culture or country? How does communal living (or by contrast independent living) impact how space is shared in the home? How would these ways of living impact the expectations of privacy among family members?
2. What would your life be like if you did not have regular access to electricity? What are some things that you would do during power outages or when the internet was not available?
3. In what ways do the use of space and the fuels we use for cooking define the culture in which we live? Are there times when people from your culture live a more communal lifestyle and make use of fuels other than electricity for cooking?

## Key Vocabulary

### *Nouns*

<b>bafu la kuogea</b>	bathtub
<b>bakuli</b>	bowl
<b>benchi</b>	bench
<b>bilauri; glasi</b>	glass
<b>birika</b>	kettle
<b>blanketi</b>	blanket
<b>bomba</b>	pipe
<b>buli</b>	teapot
<b>busati; mkeka</b>	mat
<b>chano</b>	tray
<b>choo; msalani</b>	toilet
<b>chungu</b>	earthen cooking pot
<b>chupa</b>	bottle
<b>dohani</b>	chimney
<b>feni; panka</b>	fan
<b>foronya</b>	foam pad
<b>friji; jokofu</b>	fridge; refrigerator
<b>godoro</b>	mattress
<b>jaa la takataka</b>	trash can; litter bin
<b>jiko la gesi</b>	gas stove
<b>jiko la kuni</b>	wood stove
<b>jiko la makaa; seredani</b>	charcoal stove
<b>jiko la stima</b>	electric stove
<b>jiko</b>	cooking stove
<b>joko; tanuri</b>	oven
<b>kabati</b>	cupboard; cabinet
<b>kabati la nguo</b>	wardrobe
<b>kabati la vyombo</b>	cupboard; kitchen cabinet
<b>kambarau</b>	elevator; lift
<b>karatasi; shashi</b>	tissue
<b>kaseti</b>	cassette; cd
<b>kijiko</b>	spoon
<b>kikombe</b>	cup
<b>kipandio</b>	staircase
<b>kisu</b>	knife
<b>kitanda</b>	bed
<b>kiti</b>	chair
<b>kochi</b>	couch
<b>kompyuta</b>	computer
<b>kuni</b>	firewood
<b>marashi</b>	perfume
<b>mchoro</b>	artwork
<b>meza</b>	table
<b>moto</b>	fire
<b>mrefeji</b>	tap
<b>mtu</b>	pillow; cushion
<b>mwiko</b>	wooden spoon

**nguo** cloth; clothes  
**pazia** curtain  
**picha** picture  
**rafu ya vitabu** bookshelf  
**runinga; televisheni** television  
**saa** clock  
**saa ya ukuta** wall clock  
**sahani** plate  
**sanamu** sculpture  
**shuka** bed sheet  
**simu tamba; simu ya mkono; rununu** cell phone  
**sinia** platter  
**sinki; karo** sink  
**sofa** sofa  
**susu** trivet; hot pad  
**swichi** switch  
**swichi ya feni** fan switch  
**swichi ya taa** light switch  
**taa** light; lamp  
**taulo** towel  
**ubao** cutting board  
**uma** fork  
**umeme** electricity  
**video** video  
**wimbimikro; maikrowevu** microwave  
**zulia** carpet

## Key Phrases


**Banda la gari liko karibu na nini?** What is close to the garage?  
**Chumba chako cha kulala kina vitu gani?** What things are in your bedroom?  
**Nyumba yako ina vitu gani?** What things are in your house?  
**Nyumba yako ina vyumba gani?** What rooms does your house have?  
**Sebule ya nyumba yako ina vitu gani?** What things are in your living room?  
**Unatafuta aina gani ya nyumba?** What type of house are you looking for?  
**Ungependa kuishi katika aina gani ya nyumba?** What type of house would you like to live in?

## 4.3 Nje ya nyumba



### Zoezi A

One of the sons in Shamila's host family works in Dar es Salaam but will soon be relocating to Nairobi. He comes home one weekend to share the news with his family. Read his description of the house he has found and answer the questions that follow.



Nyumba hii iko katika mtaa wa Gigiri, mjini Nairobi. Nyumba inapendeza sana na ina muundo wa kisasa na usanifu majengo wa hali ya juu. Nyumba iko katika shamba ambalo ukubwa wake ni nusu ekari. Paa la nyumba ni la vigae vya rangi nyekundu. Nyumba ina madirisha makubwa mengi. Nyumba ni ya ghorofa mbili na ina roshani katika ghorofa ya kwanza na ya pili. Roshani moja iko mbele ya nyumba. Nyumba ina bustani ndogo ya maua. Mbele ya nyumba kuna ua kubwa ambalo lina miti aina ya mikindu. Kuna lango kubwa la rangi ya kahawia la kuingia katika boma hili. Kuta za nyumba ni za rangi ya manjano. Na pia kuna barabara ya gari ambayo inaelekea nyuma ya nyumba ambapo kuna ua kubwa na pia eneo kubwa la kuegeza magari. Nje ya nyumba kuna tangi la maji ambalo liko chini ya ardhi. Kuna uzio wa mawe. Mlango wa mbele ni wa chuma na ni wa rangi nyekundu. Nyumba iko karibu na makao makuu ya Shirika la Umoja wa Kimataifa, na soko la Village Market na Ubalizi wa Marekani. Isitoshe, kuna ulinzi mkali. Pia kuna kituo cha polisi karibu, hospitali chache, kama vile MP Shah, na Aga Khan na shule nyingi za msingi na sekondari. Pia, kuna msitu wa Karura.

1. Mbele ya nyumba kuna nini?
2. Nyuma ya nyumba kuna vitu gani?
3. Nyumba ambayo Yusufu anataka kukodisha iko wapi?
4. Vigae vya nyumba na mlango wa mbele wa nyumba ni rangi gani?
5. Kuna nini nje ya nyumba?
6. Kuna huduma gani karibu na nyumba hii?
7. Kuna vitu gani nje ya nyumba yako?
8. Kuna huduma gani karibu na nyumba yako?



## Zoezi B

Over the weekend, Mwalimu Bakari will host his Kiswahili class at his home for a group dinner. Mwalimu Bakari describes the exterior of his house at the end of class so that his students can locate it easily when they arrive. Read his description and answer the questions that follow.



Nyumba yangu iko karibu na barabara ya Kitisisi. Paa la nyumba ni la vigae vya rangi nyeusi. Madirisha ya nyumba yana vioo vya kumulika. Nyumba ina baraza ndogo mbele. Baraza ni ya rangi ya machungwa. Mbele ya nyumba kuna ua kubwa. Mbele ya nyumba kuna mimea mitatu midogo ambayo imeungwa kwa uzio mdogo. Kuna lango kubwa la kuingia kwenye nyumba. Lango ni la rangi ya kijivu. Mlango wa banda la gari ni wa rangi nyeusi. Ukuta wa nyumba ni wa matofali. Nyumba yangu imezungukwa na uzio wa mawe na pia kuna miti mingi.

1. Nyumba ya Mwalimu Bakari iko wapi?
2. Paa la nyumba ya Mwalimu Bakari ni la vigae vya rangi gani?
3. Kuna nini mbele ya nyumba ya Mwalimu Bakari?
4. Nyumba ya Mwalimu Bakari imezungukwa na nini?
5. Je, kuna lango kubwa la kuingia katika nyumba ya Mwalimu Bakari?
6. Ukuta wa nyumba ya Mwalimu Bakari ni wa aina gani?
7. Rangi za nyumba yako ni zipi?



## Zoezi C

Shamila and Joseph are on their way to a classmate's house for a birthday celebration. They call their friend to ask a few questions about the exterior of the house so that they can locate it. Read their dialogue and answer the questions that follow.



**Shamila na Joseph:** Habari gani Juma?

**Juma:** Salama sana. Je, mtafika kwenye karamu?

**Shamila na Joseph:** Ndiyo. Tutafika kwenye karamu. Kwa sasa tunajaribu kutafuta nyumba yenu?

**Juma:** Je, mko wapi?

**Shamila na Joseph:** Tuko karibu na lango la kahawia? Nyumba yenu ni gani?

**Juma:** Je, mnaona nyumba ya paa la vigae vya rangi ya kahawia ambalo lina tangi la maji juu yake?

**Shamila:** Ndiyo, tunaona nyumba mbili zenye mapaa ya vigae? Je, nyumba yenu ni gani?

**Juma:** Utaona ua mkubwa wenye maua mengi. Nyumba imezungukwa na uzio wa mawe.

**Shamila na Joseph:** Sawa tumeiona. Tutaonana hivi karibuni.

**Juma:** Karibuni sana.

1. Nyumba ya Juma ina paa la vigae vya rangi gani?
2. Ua la Juma lina vitu gani?
3. Juu ya nyumba ya Juma kuna vitu gani?
4. Nyumba ya Juma imezungukwa na uzio wa aina gani ?
5. Shamila na Joseph wanaenda kufanya nini kwa nyumba ya rafiki yao?





## Zoezi D

During their stay in Tanzania, Mwalimu Bakari asks Shamila, Joseph, and the other study abroad students living with host families to briefly describe their host families' homesteads. Listen to Shamila's description of Bibi Farida and Bwana Juma's homestead while drawing a sketch of it. Then, answer the following questions.

1. Familia pokezi ya Shamila inakaa wapi?
2. Kiambo cha Bibi Farida kina nyumba ngapi?
3. Nyumba kubwa zaidi ina vyumba gani?
4. Banda la kuegesha gari liko wapi?
5. Je, nyumba hii ina choo na bafu?
6. Jikoni iko wapi?
7. Nyumba kubwa ya Bibi Farida na Bwana Juma ina rangi gani ndani na nje?
8. Bwana Juma ana mifugo ya aina gani?
9. Kiambo cha Bibi Farida na Bwana Juma kina maua ya rangi gani?
10. Uwanja wa kuchezea mpira uko wapi?

### Sarufi: Kivumishi -a-unganifu (*Connective -a- of association*)

The connective *-a* of association is used to indicate the relationship between two nouns, and it is most often translated as "of" or "s" in English, denoting possession or belonging. We have already seen it used frequently to talk about family members:

Baba **wa** Joseph anaitwa Eric.  
Familia **ya** Shamila ni kubwa.

*Joseph's father is called Eric.  
Shamila's family is big.*

The prefix of *-a* of association changes based on the noun class of the person or thing being "possessed" or described. Note that it is possible to use one or two associatives in a sentence.

Habari **za** familia?  
*How is the family?*

Shamila anasoma katika Chuo kikuu **cha** Kansas.  
*Shamila studies at the University of Kansas.*

Kitabu **cha** Kiswahili kimefika.  
*The Kiswahili book has arrived.*

Vitabu **vya** Kiswahili vimefika.  
*The Kiswahili books have arrived.*

The *-a* of association is also used with colors and with building materials.

Kuna kochi **la** rangi **ya** kahawia katika sebule.  
*There is a brown couch **in** the living room.*

Nyumba yenye kuta **za** kijani ni **ya** mwalimu wangu.  
*The house **with** green walls is my teacher's.*

Ukuta **wa** nyumba ni **wa** matofali.  
*The wall **of** the house is (made) **of** bricks.*


Keep in mind, however, that not all colors require the use of the *-a-* of association. The words for black, white and red usually agree with the nouns they modify.

Kiti cheusi kimevunjika.  
*The black seat is broken.*


Kitanda chekundu ni cha shangazi yangu.  
*The red bed is my aunt's.*

Nguo nyeupe imeoshwa.  
*The white cloth has been washed.*


The following are the common colors in Kiswahili.




nyeupe  
(white)




nyeusi  
(black)




nyekundu  
(red)



kijani  
(green)




kijivu  
(gray)




manjano  
(yellow)




zambarau  
(purple)




buluu  
(blue)




kahawia  
(brown)



dhahabu  
(gold)



machungwa  
(orange)



waridi  
(pink)



## Zoezi E

Complete the following sentences using the appropriate *-a* of association from the word bank below.

wa | ya | cha | vya  
ya | za | la | pa | kwa

1. Mtoto \_\_\_\_\_ mwalimu ni mgonjwa.
2. Kiti \_\_\_\_\_ Juma ni \_\_\_\_\_ rangi ya kahawia.
3. Mlango \_\_\_\_\_ nyumba yake ni \_\_\_\_\_ rangi \_\_\_\_\_ kijivu.
4. Vioo \_\_\_\_\_ nyumba yake vimevunjika.
5. Nyumba \_\_\_\_\_ mabati zinadumu sana.
6. Sahani \_\_\_\_\_ Amina ni nzuri sana.
7. Wasichana \_\_\_\_\_ mama Mwajuma wanakaa Marekani.
8. Pahali \_\_\_\_\_ kununua chakula ni pazuri sana.
9. Mbwa \_\_\_\_\_ kaka ni mkubwa.
10. Darasa letu \_\_\_\_\_ Kiswahili ni dogo.



## Zoezi F

Complete the following sentences with the correct form of the connective *-a* of association.

1. Mtoto \_\_\_\_\_ mama amefika.
2. Chumba \_\_\_\_\_ maakuli ni kizuri.
3. Kijiko \_\_\_\_\_ mtoto ni kipya.
4. Nyumba \_\_\_\_\_ mwalimu Bakari ni kubwa.
5. Viatu \_\_\_\_\_ baba ni vyeusi.
6. Gari \_\_\_\_\_ mama ni \_\_\_\_\_ rangi nyekundu.
7. Vyumba \_\_\_\_\_ kulala ni vikubwa.
8. Nyumba yake imepakwa rangi \_\_\_\_\_ buluu kwenye ukuta.
9. Mji \_\_\_\_\_ Nairobi ni \_\_\_\_\_ kupendeza.
10. Chuo kikuu \_\_\_\_\_ Kansas ni \_\_\_\_\_ wanafunzi wazuri.



## Zoezi G

Answer the following questions. Then, take turns asking one or two classmates the same questions. Be prepared to report your responses to the class.

1. Paa la nyumba yako ni la rangi gani?
2. Kuta za ndani ya nyumba yako ni za rangi gani?
3. Milango ya nyumba yako ni ya rangi gani?
4. Dari la nyumba yako ni la rangi gani?

### Sarufi: Vihusishi (*Prepositional phrases*)

A preposition is a word that indicates the relationship between a noun and other words in the sentence. One of the more common uses for prepositions is to indicate the location of an object. For example, “The book is *in* the living room,” where *in* indicates where the book is located, or, “The book is *on* the table *next to* the remote control”, in which *on* and *next to* indicate the spatial relationship of the two objects.

Below is a list of common Kiswahili prepositional phrases to describe the relative position of objects.

baada ya	<i>after</i>
chini ya	<i>underneath; below</i>
juu ya	<i>on top of; about; above</i>
kabla ya	<i>before</i>
kando ya	<i>beside; along</i>
karibu na	<i>close to; near</i>
karibu	<i>around; near</i>
kati ya; baina ya	<i>between</i>
katikati ya	<i>in between</i>
kisha	<i>then; and then</i>
kwenye; katika	<i>toward; on; in; inside</i>
mbali na	<i>far from; far</i>
mbele ya	<i>in front of</i>
mpaka; hadi	<i>until; ‘til</i>
ndani ya	<i>inside of; in</i>
nje ya	<i>outside of</i>
nyuma ya	<i>behind</i>
tangu; toka; kutoka	<i>from; since</i>

The verb **kuna** (there is) is often used alongside these prepositions.

**Kuna** kidimbwi cha kuogelea **nje ya** nyumba.  
**There is** a swimming pool **outside** the house.

**Kuna** miti **mbele ya** nyumba yake.  
**There are** trees **in front of** his house.

**Kuna** rafu ya vitabu **karibu na** dirisha.  
**There is** a bookshelf **near** the window.

**Kuna** viti vingi **ndani** ya sebule.  
*There are many seats in the living room.*

**Kuna** wanafunzi wachache **nje** ya darasa.  
*There are few students outside the classroom.*



### Zoezi H

Working in pairs, describe the image below (listing the names of items, their locations, colors, etc.). Practice asking one another questions about things in the room.

#### **Example:**

Kuna nini mbele ya kochi?  
*What is in front of the couch?*

Kuna meza ndogo ya mbaao mbele ya kochi.  
*There is a small wooden table in front of the couch.*

Maua ambayo yako juu ya meza ni ya rangi gani?  
*What is the color of the flowers that are on top of the table?*



### Zoezi I

Choose one room of your house and describe it in detail. Be sure to describe the location of items and their colors. If possible, provide an image of the room along with the description.



### Zoezi J

You have arrived at your friend's house to visit, but you are not entirely sure you are at the right house. Call your friend and ask them at least five questions about the exterior of the house to make sure that you are at the right house.



### Zoezi K

Working in groups, find a house on the internet that is unique and interesting. Prepare a description of the interior and exterior of the house to present to the class.



### Zoezi L

You will be hosting a party next weekend. Text the friends you are inviting to give them details for the party (e.g., day, time, and a description of the exterior of your house so that they can identify it easily when they arrive).



### Zoezi M

Read the party descriptions prepared by your classmates in the activity above and then discuss which party you are likely to attend.



### Zoezi N

Listen to the conversation between Shamila and her host mother about the exterior of houses in East Africa and the U.S. Then, complete the chart below with details of their similarities and differences.

Vitu gani sawa?	Vitu gani ni tofauti?



## Zoezi O

After describing their host families' houses, Mwalimu Bakari asked the students to write a short essay to illustrate how the houses in East Africa differ with those in their home country. Read Joseph's comparison below and answer the questions that follow.

Jina langu ni Joseph, mimi ninatoka nchi ya Marekani, lakini kwa sasa ninaishi na familia yangu pokezi katika mtaa wa Kinondoni, mjini Dar es Salaam. Familia hii inaishi karibu na kanisa kuu la Azania Front. Wao wana nyumba kubwa ambayo ina vyumba vinne. Kuna tofauti kidogo kati ya nyumba hii ya familia yangu pokezi na nyumba za nchi ya Marekani. Kwanza kabisa, nyumba hii ina vyumba vichache kuliko nyumba yangu ya Marekani. Katika nyumba hii kuna vyumba viwili vya kulala, sebule na chumba cha maakuli. Katika nyumba hii hakuna jikoni, choo na bafu kama nyumba za Marekani. Jikoni iko nje ya nyumba lakini Marekani jikoni iko ndani ya nyumba. Pia familia hii wanatumia choo cha shimo, choo kiko nyuma ya nyumba.

Isitoshe, katika nyumba hii hakuna pahali pa kuoshea nguo kama nyumba za Marekani. Bibi Farida hufua nguo kwa mikono nje ya nyumba. Katika nyumba ya familia yangu hakuna maji ndani ya nyumba. Wao huteka maji kwenye kisima ambacho kiko nje ya nyumba. Paa la nyumba ya familia yangu limeezekwa kwa makuti. Hii, ni tofauti na nyumba nyingi za Marekani ambazo zimeezekwa kwa vigae. Sakafu ya nyumba ni ya saruji na hakuna zulia kama nyumba nyingi za Marekani.

Katika nyumba hii, kila chumba kina rangi tofauti lakini nyumba nyingi za Marekani nyumba zina rangi moja tu. Katika nyumba ya Bibi Farida, vyumba vyote vya kulala vina rangi ya kijani, sebule ina rangi ya waridi na chumba cha maakuli kina rangi ya manjano kwenye ukuta.

1. Joseph anatoka nchi gani?
2. Familia pokezi ya Joseph wanaishi wapi?
3. Nyumba ya Bibi Farida ina vyumba vingapi?
4. Je, katika nyumba hii kuna pahali pa kufua nguo?
5. Sakafu ya nyumba ya Bibi Farida ni ya aina gani?
6. Vyumba vya nyumba ya Bibi Farida vina rangi gani?
7. Kuna tofauti gani kati ya nyumba ya familia pokezi na nyumba ya familia ya Joseph ya Marekani?
8. Eleza kuhusu nyumba ya familia yako.





## Zoezi P

Listen to the description of Bibi Fatuma's house and answer the questions below.

1. Bibi Fatuma na familia yake wanaishi wapi?
2. Nyumba ya Bibi Fatuma ina vyumba vingapi?
3. Vyumba vya kulala vina rangi gani?
4. Chumba cha maakuli na sebule ni rangi gani?
5. Jikoni mna rangi gani?
6. Sakafu na dari ni za rangi gani?
7. Ukuta wa nje una rangi gani?

## Cultural Explorations

In rural East Africa, houses are built out of materials that are most readily available. Most rural houses are round with mud walls and a roof that is either thatched or covered with iron sheets; others may be built of wood or papyrus reeds, if available. Houses made of wood or concrete are generally painted. Those made of mud are often adorned with decorative clay applied with specific designs and often changed on a seasonal basis. Most homesteads are surrounded by fences, usually made of wood and barbed wire. One might also see a live hedge or flowers that may be distinctive in some way. More recently, peri-urban areas have started building multi-story buildings out of concrete blocks and with roofing tiles to mirror building styles more common in urban areas.



As most houses do not have house numbers, there is a greater need to create a distinctive exterior that can be easily described. It is, as such, quite commonplace to describe the features of the exterior of the house or building (e.g., the number of floors, the type and color of roof, the type of gate, the color of the walls, etc.) rather than just give someone an address. The same generally holds true for apartment complexes, which have no numbers on the building(s) or the individual apartments. Because of this, directions will include specific details on location (e.g., third building from the entrance, second floor, first apartment on the right with a red door, etc.). These descriptions are crucial for visiting guests, for vendors delivering groceries or other goods, or for taxi drivers picking up or dropping off passengers.



While urban areas do have street names for the most part, in smaller towns only the main streets are named. In very rural areas, there may not be street names at all. Be prepared for detailed directions if you are visiting friends outside of a major city.



Letters and packages are usually not delivered to the recipient's home unless you pay an extra fee. Instead, mail is picked up at the town's central post office where the recipient can retrieve their mail from a personalized post office box or courier company offices. Packages can also be sent through public transport companies, but again, these packages are not sent to the recipient's home. These packages must be picked up from the shipping company's local office, with proof of identification to retrieve the package.

### **Cultural Reflections:**

With a classmate or in a small group, discuss the cultural information you have just read by answering the questions below.

1. How are the exteriors of homes decorated in your neighborhood or town? Is this trend consistent or similar to that of your nation? How does this compare to the decorations and distinct designs on the exteriors of East African homes?
2. What are some common building materials for housing in your region? Are these materials similar to those used nationwide? How do these materials compare to those used in East Africa?
3. With the precautions put in place due to COVID-19, many nations saw an increase in the amount of goods delivered to residences. Imagine how a similar system could work in East Africa where goods are not usually delivered to homes, especially in rural areas.



**Zoezi Q**

Write a short essay to illustrate similarities and differences between housing in East Africa and in your country.

## Key Vocabulary

### *Colors*

<b>bluu; samawati; samawi</b>	blue
<b>dhahabu; zari</b>	gold
<b>-ekundu</b>	red
<b>-eupe</b>	white
<b>-eusi</b>	black
<b>fedha</b>	silver
<b>hudhurungi</b>	mustard
<b>kahawia</b>	brown
<b>kijani; kibichi</b>	green
<b>kijivu</b>	gray
<b>machungwa</b>	orange
<b>manjano</b>	yellow
<b>maziwa</b>	milky white
<b>nili; bluu giza</b>	indigo
<b>rangi ya giza</b>	dark color
<b>rangi ya mwangaza</b>	light color
<b>rangirangi</b>	multicolored
<b>samli</b>	off white
<b>shaba</b>	bronze
<b>urujuani</b>	violet
<b>waridi</b>	pink
<b>zambarau</b>	purple

### *Nouns*

<b>almasi</b>	diamond
<b>baraza</b>	veranda
<b>bustani</b>	yard (American); garden (British)
<b>dari</b>	ceiling
<b>dirisha</b>	window
<b>gereji; banda la gari</b>	garage
<b>ghala</b>	granary
<b>kiambo</b>	village; compound
<b>lango</b>	gate
<b>mabati</b>	iron sheets for roofing
<b>makuti</b>	palms
<b>mawe</b>	stone
<b>mlango</b>	door
<b>nyasi</b>	grass
<b>paa</b>	roof
<b>pazia</b>	curtain
<b>rangi</b>	color
<b>roshani</b>	balcony
<b>sakafu</b>	floor
<b>shamba</b>	farm
<b>ua</b>	courtyard; compound; fence
<b>ukuta</b>	wall
<b>uwanja</b>	field

**uzio** fence; hedge  
**vigae** tiles  
**zizi** cowshed

#### *Verbs*

**-ezeka** to roof  
**-paka** to paint  
**-panga** to arrange  
**-weka** to put

### **Key Phrases**

**Vyumba katika nyumba yako vina rangi gani?** What are the colors of rooms in your house?

**Makochi yako ni ya rangi gani?** What is the color of your couches?

**Nyumba yako imezekwa na nini?** What is your roof made of?

**Sakafu ya nyumba yako ni ya aina gani?** What type of floor does your house have?

**Friji iko wapi kwenye nyumba yako?** Where is the fridge located in your house?

**Kuna nini kwenye ukuta wa nyumba yako?** What do you have on the wall of your house?

**Televisheni iko wapi kwenye nyumba yako?** Where is the television located in your house?

**Kizingiti cha viatu kiko wapi kwenye nyumba yako?** Where is the shoe rack located in your house?


## 4.4 Mtaa na ujirani



### Zoezi A

For one of their assignments, the Kiswahili students were asked to give presentations describing where they live using photos of key landmarks. Below are transcripts of Shamila and Joseph's presentations. Read them and answer the questions that follow.

*Shamila describes her neighborhood*



Mimi ninaishi mjini pamoja na familia yangu pokezi, Bwana Juma na Bibi Farida. Tunaishi karibu na soko la samaki la Mzizima. Hili ni eneo la makazi ambalo lina nyumba nyingi na watu wengi pia. Soko hili liko maili tano kutoka nyumbani kwa familia pokezi na ni maarufu kwa uuzaji wa samaki. Mimi na Bibi Farida, huenda sokoni kila wikendi kununua samaki. Kuna sehemu kubwa ambayo ni soko la wazi ambalo liko karibu na bahari. Wavuvi huvua samaki baharini na kuwauza katika soko la wazi. Pia soko hilo lina majengo mawili ambayo yako katika ghorofa ya chini. Kuna soko la ndani kubwa ambalo limegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni ghorofa ya kwanza, sehemu ya kati na ya chini.

Ingawa eneo la Mzizima limezungukwa na maduka yanayouza bidhaa mbalimbali, bado soko la Mzizima ndilo soko kuu la mauzo ya samaki na bidhaa za kilimo nchini. Linauza mazao kwa bei ya jumla na ya rejareja pamoja na vifaa vya kilimo. Majengo mengine maarufu katika soko hili ni Jumba la Natwar. Hili ni jengo la kumbukumbu. Jengo hili lilijengwa wakati wa ukoloni na lina msikiti mkubwa sana. Wakazi, wageni na wafanyabiashara huabudu katika msikiti huu. Mtaa huu ni safi sana, salama na maridadi. Kuna kituo cha polisi, kwa hivyo polisi huimarisha hali ya usalama sokoni kila wakati.

1. Soko la samaki liko umbali gani na familia pokezi ya Shamila?
2. Kwa nini Shamila na Bibi Farida huenda soko la Mzizima kila wikendi?
3. Soko la wazi la Mzizima ni maarufu kwa vitu gani?
4. Soko la Mzizima lina majengo yapi makuu?
5. Jengo la Natwar lilijengwa wakati gani?
6. Wakazi, wafanyabiashara na wageni katika eneo la Mzizima huabudu wapi?
7. Kwa nini hali ya usalama ni nzuri katika eneo la Mzizima?

*Joseph describes his neighborhood:*

Nyumba ya familia yangu pokezi iko karibu na kanisa kuu la Azania Front. Kanisa hili liko katikati mwa mji wa Dar es salaam ambao ni maarufu sana kwa watalii. Kanisa pia lipo karibu na bahari. Kanisa hili ni la dini ya Kilutheri. Kanisa kuu la Azania Front lipo maili mbili kutoka nyumbani kwa Bwana Musa. Kanisa hili lilijengwa na wamishonari Wajerumani mwaka wa elfu moja mia nane na tisini na nane. Kanisa hili lina paa la vigae vya rangi nyekundu na limezungukwa na uzio mfupi ulio na mapambo ya misalaba. Nje ya jengo la kanisa kuna aina mbalimbali ya miti. Karibu na kanisa kuna majengo mengine kama vile ofisi za serikali, majumba ya biashara, benki na kadhalika. Karibu na kanisa la Azania Front kuna kituo cha polisi na hospitali ya umma.

Kila Jumamosi mimi, Masika, na Chacha huenda kupumzika karibu na mto wa Wami. Mto huu uko umbali wa kilomita ishirini kutoka nyumbani kwa familia pokezi yangu. Mto huu uko ufukweni na uko karibu na hifadhi ya msitu wa Pugu. Mara kwa mara sisi hupenda kufanya mazoezi na kukwea mlima ulioko katika msitu wa Pugu kwa sababu ni salama na hakuna wanyama hatari wa porini. Humo kwenye msitu wa Pugu kuna mto pia.



1. Kuna vivutio gani karibu na Mto wa Wami?
2. Kanisa la Azania Front lilijengwa na nani na lilijengwa mwaka gani?
3. Kanisa kuu la Azania Front liko maili ngapi kutoka nyumbani kwa familia pokezi ya Joseph?
4. Kuna majengo gani mengine karibu na kanisa la Azania Front?
5. Joseph na Masika hupenda kufanya nini wanapokwenda katika Mto wa Wami?
6. Uzio ambao umezunguka kanisa una aina gani ya mapambo?
7. Kwa nini msitu wa pwagu ni salama?
8. Joseph na wenzake wanapenda kufanya nini katika msitu wa Pugu?



### Zoezi B

Listen to Shamila and Joseph's descriptions of their neighborhoods in the U.S. and answer the questions that follow.

1. Shamila na jamaa yake wanakaa katika mtaa gani?
2. Kuna vitu gani nje ya nyumba katika mitaa hii?
3. Je, kuna maduka au soko karibu na mitaa hii?
4. Joseph na familia yake wanakaa katika mtaa gani?
5. Mtaa wa Joseph una idadi gani ya watu?
6. Kuna aina gani za shule katika mtaa wa Shamila?
7. Kuna sehemu gani nyingine katika mtaa wa Encino?
8. Mtaa wa Encino una sifa gani?
9. Wewe unakaa katika mtaa gani?
10. Kuna vitu gani katika mtaa wako?



### Zoezi C

In pairs, describe the street that you live on. Be as detailed as possible so that your classmate can get the visual image of the street.



### Zoezi D

Describe your neighborhood to a classmate. Be as detailed as possible so that you can give a report about your classmate's neighborhood to the class.



### Zoezi E

A new student from East Africa is moving to your city to attend your college, and they need help finding housing. They would like to know some information about the neighborhood where you live, or perhaps information about a popular area where other undergraduate students live. In pairs, role-play this scenario pretending that one of you is the new student from East Africa and the other is from the U.S.

## Sarufi: Ngeli za mahali *-ko/-po/-mo* (Locative noun classes *-ko/-po/-mo*)

In Kiswahili, there are three noun classes that denote location. Location is expressed by the following:

- **-ko** to denote a general or indefinite place, making it the most commonly used form
- **-po** to express a more specific or definite location when the general location is known
- **-mo** to indicate location inside of something or inside of some place

Location can be expressed in various ways – locatives and noun classes or locatives and personal pronouns. The use of *-ko* and *-po* is dependent on context, so let's look at a few carefully structured examples:

<b>Uko</b> wapi sasa?	<i>Where are you now?</i>
<b>Niko</b> nchini Kenya.	<i>I am in Kenya.</i>
<b>Upo</b> wapi nchini Kenya?	<i>Where (exactly) are you in Kenya?</i>
<b>Nipo</b> mjini Nairobi.	<i>I am in Nairobi.</i>

The dialogue above would most likely be over the phone. In the first question, the person is asking for a general location and therefore uses *-ko*; the response provides a general location and uses the same locative suffix. In the second question, the person knows the general location, and so they ask for greater specificity using the suffix *-po*. If they had already known that the other person was traveling around Kenya, they could simply have asked *Upo wapi sasa?*

Let's look at another example:

<b>Uko</b> wapi sasa?	<i>Where are you right now?</i>
<b>Niko</b> chuoni.	<i>I'm on campus.</i>
Je, <b>uko</b> wapi chuoni?	<i>Where are you on campus?</i>
<b>Nimo</b> maktabani.	<i>I am in the library.</i>

These questions are all requests for a general location, with the last answer reflecting an interior location, and thus using the prefix *-mo*. If the first person decides to go to the library to find the other person, we would get an exchange like this:

<b>Nimo</b> maktabani. <b>Upo</b> wapi?	<i>I am in the library. Where (exactly) are you?</i>
<b>Nipo</b> kwenye ghorofa ya tatu karibu na ngazi.	<i>I am on the third floor near the stairs.</i>

Remember that *-ko* is used to give a general location and is the most frequently used. You will only use *-po* if the general location is known but more specific information is needed.

Funguo zangu <b>zipo</b> wapi?	<i>Where are my keys?</i>
Kitabu changu <b>kipo</b> wapi?	<i>Where is my book?</i>

To this point, you have been using the verb *kuna* to describe the location of objects. For example:

**Kuna** meza ndogo mbele ya kochi.      **There is** a small table in front of the couch.  
**Kuna** kitabu cha kijani juu ya meza.      **There is** a green book on the table.

Those same descriptions can be written in a slightly different way using these *-ko/-po/-mo* suffixes.

Meza ndogo **iko** mbele ya kochi.      *A small table is in front of the couch.*  
Kitabu cha kijani **kiko** juu ya meza.      *The green book is on the table.*  
Vyombo **vimo** ndani ya kabati.      *The utensils are in the cupboard.*  
Wanafunzi wapo shuleni.      *The students are in school.*



## Zoezi F

Look at the *kuna* sentences below and convert them to sentences with *-ko/-po/-mo* locatives. Pay attention to the context in choosing the correct suffix.

### Example:

Kuna miti mingi mbele ya nyumba.  
Miti mingi **iko** mbele ya nyumba./ Miti mingi **ipo** mbele nyumba.

1. Kuna simu ndani ya mkoba.  
\_\_\_\_\_
2. Kuna vitabu vingi kwenye rafu.  
\_\_\_\_\_
3. Kuna wanafunzi ndani ya darasa.  
\_\_\_\_\_
4. Kuna watoto wengi kwenye uwanja wa shule.  
\_\_\_\_\_
5. Kuna wanafunzi katika chuo kikuu sasa kwa sababu hali ya hewa ni nzuri.  
\_\_\_\_\_
6. Kuna vitu vingi vya matumizi ya jikoni kwenye soko.  
\_\_\_\_\_
7. Kuna kalamu mbili juu ya meza ndani ya ofisi ya mwalimu.  
\_\_\_\_\_
8. Kuna walimu wengi katika ofisi.  
\_\_\_\_\_
9. Kuna tangi nyingi juu ya nyumba.  
\_\_\_\_\_





## Zoezi G

Write five of your own sentences using *-ko/-po/-mo* to describe the relative location of items in the classroom. Be prepared to share your sentences with the class.

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

## Sarufi: *-ni ya mahali (Locative suffix -ni)*

When making general comments about location, one can also add the suffix *-ni-* in place of a preposition (*katika*, *ndani ya*, *kwenye*) to indicate that something is inside.

Wanafunzi wako chuoni.  
*The students are on campus.*

Vyombo viko kabatini.  
*The utensils are in the cupboard.*

Kompyuta zimo maktabani.  
*The computers are in the library.*

Remember that you cannot use the prepositions *katika*, *ndani ya*, or *kwenye* with *-ni-* since they all denote “inside”.

Also note that *-ni-* cannot be used with proper nouns, such as the names of cities and countries. In those cases, you must use the prepositions *katika* or *kwenye*:

Joseph anaishi **katika** nchi ya Tanzania.  
*Joseph lives **in** Tanzania.*

Joseph anaishi **kwenye** nchi ya Tanzania.  
*Joseph lives **in** Tanzania.*



## Zoezi H

Work with a classmate to rewrite the sentences in *Zoezi F* using the locative suffix *-ni-* in place of the prepositional phrase. If you finish early, try rewriting the sentences that you created for *Zoezi G*.



## Zoezi I

Complete the sentences using the locative markers provided below.

**kiko | liko | mjini | nyumbani | sokoni**  
**uko | vimo | vipo | wamo | yuko | yumo**

1. Shamila na Bibi Farida hupenda kwenda \_\_\_\_\_ Mzizima katika mji wa Dar es Salaam kununua vyakula.
2. Joseph anaishi \_\_\_\_\_ mwa Bwana Musa na Bibi Fatuma.
3. Kanisa \_\_\_\_\_ maili mbili kutoka nyumbani kwa Bwana Musa.
4. Mto wa Wami \_\_\_\_\_ mbali na kanisa kuu la Azania Front.
5. Bwana Musa hupenda kwenda kutembea \_\_\_\_\_.
6. Vikombe na vijiko \_\_\_\_\_ kabatini.
7. Visu vya kulia mezani \_\_\_\_\_ juu ya meza katika chumba cha maakuli.
8. Wanafunzi wengi \_\_\_\_\_ darasani, kwa hivyo mwalimu atianza kufundisha.
9. Baba \_\_\_\_\_ ofisini anafanya kazi.
10. Kitanda cha mtoto \_\_\_\_\_ karibu na dirisha.



## Zoezi J

After getting to campus one morning, Shamila realizes that her laptop is not in her backpack. She calls Bibi Farida and asks her to check several places in the house to see if the laptop is still there. Read their conversation and answer the questions that follow.

**Shamila:** Shikamoo Bibi Farida?

**Farida:** Marahaba Shamila. Habari za masomo leo?

**Shamila:** Salama tu. Je, uko nyumbani ama ushaondoka kuelekea kazini?

**Farida:** Bado niko nyumbani. Nitaondoka baada ya nusu saa. Unahitaji chochote?

**Shamila:** Kompyuta yangu haimo mkobani. Sijui kama nimeisahau nyumbani? Tafadhali angalia kama imo chumbani mwangu mwa kulala.

**Farida:** Sawa. Subiri kidogo. Haimo chumbani. Haipo juu ya meza wala juu ya kitanda.

**Shamila:** Je, ipo kwenye rafu ya vitabu?

**Farida:** Ndiyo, ipo kwenye rafu ya vitabu.

**Shamila:** Hizi ni habari njema. Nina furaha kuwa ipo nyumbani. Nilikuwa na wasiwasi sana. Nilifikiri kuwa imepotea.

1. Bibi Farida alikuwa wapi Shamila alipompigia simu?
2. Bibi Farida aliitafuta kompyuta ya Shamila wapi?
3. Bibi Farida aliipata kompyuta ya Shamila wapi?
4. Kwa nini Shamila alikuwa na wasiwasi?



## Zoezi K

Joseph calls his friend Yusufu one Saturday afternoon to see if he wants to go to the mall downtown. Listen to their conversation and answer the questions that follow.

1. Joseph anataka kwenda wapi?
2. Joseph anataka kwenda kufanya nini mjini?
3. Yusufu yuko wapi?
4. Yusufu anafanya nini sasa?
5. Yusufu na Joseph watakutana wapi mjini?



## Zoezi L

Assume that you and a classmate will be studying abroad next summer. You would like to share an apartment or house to reduce living expenses. Read the advertisements below and pick the place that you would like to rent. Be ready to explain your choice to the class.

**KODI:** TSh 250,000 kwa mwezi.

**NYUMBA IKO WAPI?:** Kinondoni, Mabwemanda, Dar es Salaam.

**AINA YA NYUMBA:** Nyumba ya kukodisha.

**UNAWEZA KUPIGA BEI?:** Ndiyo.

**MASHARTI:** Unaomba nyumba miezi sita kabla ya kuingia. Unahitaji kulipa kodi ya miezi mitatu kabla ya kuingia.

**IDADI YA VYUMBA VYA KULALA:** 2.

**IDADI YA MISALA:** 2.

**VIFAA:** Kidimbwi cha kuogelea, chumba cha mazoezi, duka la vyakula, duka la maji, chumba cha kuoshea nguo na uwanja wa watoto wa kuchezea.

**MAELEZO:** Nyumba hii ni kubwa. Iko katika mtaa wa Mabwemanda. Iko karibu na kituo cha basi. Kuna umeme na maji. Nyumba ina ua mzuri.

---

**KODI:** TSh 4,173,000 kwa mwezi.

**NYUMBA IKO WAPI?:** Kinondoni, Masaki, Dar es Salaam.

**AINA YA NYUMBA:** Fleti za kukodisha kwa muda mfupi.

**UNAWEZA KUPIGA BEI?:** Ndiyo.

**MASHARTI:** Unalipa kodi mwanzoni mwa mwezi.

**IDADI YA VYUMBA VYA KULALA:** 2.

**IDADI YA MISALA:** 2.

**VIFAA:** Nyumba ina Kiyoyozi, ina kila kitu cha nyumba, jenerata, chumba cha mazoezi, dimbwi la kuogelea, maji safi, na huduma za ulinzi.

**MAELEZO:** Unaweza kukaa katika nyumba hii kwa muda mfupi kati ya mwezi mmoja hadi miezi sita. Nyumba inapendeza na iko karibu na benki, maduka na pwani.

---

**KODI:** TSh 2,500,000 kwa mwezi.

**NYUMBA IKO WAPI?:** Kinondoni, Masaki, Dar es Salaam.

**AINA YA NYUMBA:** Fleti.

**UNAWENZA KUPIGA BEI?:** Ndiyo.

**MASHARTI:** Unahitaji kutuma maombi ya nyumba miezi sita kabla ya kuingia

**IDADI YA VYUMBA VYA KULALA:** 2.

**IDADI YA MISALA:** 2.

**VIFAA:** Kiyoyozi, ina kila kitu cha nyumba, jenerata na huduma za ulinzi.

**MAELEZO:** Hii ni nyumba ya kisasa ambayo ina sebule kubwa. Nyumba imetunzwa vizuri sana. Nyumba ina vyumba viwili vya kulala na jikoni kando. Msalani kuna choo pamoja na bafu. Piga simu au tuma ujumbe kwa Whatsapp ili tupange kukuonyesha nyumba.

---

**KODI:** TSh 2,760,000 kwa mwezi.

**NYUMBA IKO WAPI?:** Ilala, Upanga Magharibi, Dar es Salaam.

**AINA YA NYUMBA:** nyumba ya ghorofa ya kisasa.

**UNAWENZA KUPIGA BEI?:** Ndiyo.

**IDADI YA VYUMBA VYA KULALA:** 4.

**IDADI YA MISALA:** 3.

**VIFAA:** Kiyoyozi, mashine ya kuoshea nguo, na mashine ya kuoshea vyombo.

**MAELEZO:** Nyumba hii inapendeza sana. Nyumba ina vyumba vinne vya kulala, sebule kubwa, chumba cha maakuli, jikoni. Kuna makazi ya wafanyikazi na maeneo matano ya kuegesha gari. Piga simu sasa ili tuweze kukuonyesha nyumba hii.

---

Ukiwa na maswali kuhusu nyumba yoyote unaweza piga simu au kutuma ujumbe kwa Whatsapp kwa nambari hii.

**NAMBARI YA SIMU:** +255 774 6789871.

Barua pepe: [zotechrealestate.org](http://zotechrealestate.org)



## Zoezi M

You would like to know more about the neighborhood where the rental property that you selected is located. Prepare a short list of questions that you might ask the real estate agent.



## Zoezi N

Do some research on your own to find out more about the neighborhood in Dar es Salaam where the rental property is located. You might even have a look at the city using Google Maps to get a sense of what kind of shopping, dining, and transportation options exist. Using this additional information, write an email to the real estate agent explaining which apartment you would like to rent and what you like about it. Include any questions that you might have pertaining to the property.

## Cultural Explorations

Within rural areas in East Africa, villages are formed of a collection of homesteads. Village elders handle issues like allocating water usage and settling minor disputes, such as land disputes, and may also be tasked with administering other services (e.g., security, schools, health facilities, etc.). Villages are then organized into wards, sublocations, locations, division and districts, with the largest village typically serving as the market center where people come to buy and sell goods.



In more urban areas, the city center is almost exclusively commercial buildings and stores. This is where you will find commercial shopping centers and open-air markets, as well as amenities like swimming pools, churches, institutions of higher education, museums and hotels. As one might expect, similar businesses tend to operate in close proximity to one another; property values also influence the location of certain businesses, with high-end shopping and professional services often focused on certain parts of the city center.

Residential housing is largely located within a short drive from the city center. Most people live in gated communities and pay monthly fees to cover the costs of security, garbage pickup, and maintenance of shared areas. There may be some small stores and restaurants within such a community for convenience, but the vast majority of purchases require a trip to the city center or the nearest market center. While some people own their own cars, most people walk or rely on public transportation to get to and from the city center.





### **Cultural Reflections:**

1. How much time per week do you spend shopping for food? How far do you have to travel to reach the grocery store or market?
2. Are there specific services that are only located downtown where you live? Are there specific reasons that you need to go downtown, or can you largely avoid downtown?
3. Does the neighborhood or building in which you live have services like maintenance of shared spaces or community security?

## Key Vocabulary

### *Adjectives*

<b>-baya</b>	bad
<b>-chafu</b>	dirty
<b>-dogo</b>	small
<b>-enye kelele</b>	noisy
<b>-enye nafasi kubwa</b>	spacious
<b>-enye nafasi ndogo</b>	not spacious
<b>-enye shughuli nyingi</b>	busy
<b>-enye watu wachache</b>	less densely populated
<b>-enye watu wengi</b>	densely populated
<b>fahari</b>	luxurious
<b>-fupi</b>	short
<b>ghali</b>	expensive; exorbitant
<b>haba</b>	few
<b>hatari</b>	dangerous
<b>-kubwa</b>	big
<b>maridadi</b>	beautiful
<b>-pya</b>	new
<b>rahisi</b>	cheap
<b>-refu</b>	tall
<b>safi</b>	clean
<b>starehe</b>	comfortable
<b>tele</b>	plenty
<b>-tulivu</b>	quiet
<b>-zee</b>	old
<b>-zuri</b>	good; nice; beautiful

### *Nouns*

<b>bawabu</b>	security guard; door keeper
<b>bwawa</b>	swimming pool
<b>chuma</b>	metal
<b>duka</b>	shop
<b>kanisa</b>	church
<b>kata</b>	ward
<b>kata kubwa</b>	location
<b>kata ndogo</b>	sub-location
<b>kaunti</b>	county
<b>kiduka; kioski</b>	kiosk
<b>kijiji</b>	village
<b>kijijini</b>	rural
<b>kitongoji</b>	small village
<b>kituo cha polisi</b>	police station
<b>kiunga</b>	suburb
<b>lango la kuingia</b>	entrance
<b>lango la kutoka</b>	exit
<b>majengo ya kibiashara</b>	business buildings
<b>makavazi</b>	museum
<b>makuti</b>	papyrus reeds



**mji** city  
**mjini** urban  
**mkahawa** restaurant  
**mkoa** province  
**msikiti** mosque  
**msitu** forest  
**mtaa** neighborhood  
**soko la wazi** open air market  
**takataka** garbage  
**tarafa** division  
**udongo** dirt  
**usalama** safety; security  
**usalama; ulinzi** security  
**vifaa** instruments; device; tool; gadget; amenities  
**wilaya** district

## Key Phrases

**Bei ya nyumba ni rahisi.** The rent is cheap.  
**Hali ya usalama iko vipi katika mtaa huu?** How is the security in the neighborhood?  
**Huu ni mji mdogo.** This is a small city.  
**Huu ni mji mkubwa.** This is a big city.  
**Je, kuna nyumba za kukodisha?** Are there rental houses?  
**Je, nyumba ina vyumba gani?** Which rooms are in the house?  
**Je, nyumba ina vyumba vingapi?** How many rooms are in the house?  
**Je, unaweza kupiga bei?** Can you bargain?  
**Kodi ya nyumba ni gani?** How much is the rent?  
**Kuna huduma gani katika mtaa huu?** What services are available in the neighborhood?  
**Kuna usalama wa kutosha.** There is adequate security.  
**Nyumba iko wapi?** Where is the house located?

## 4.5 Kukodisha nyumba



### Zoezi A

Shamila comes across the following rental advertisement in a local newspaper. Read the advertisement and answer the questions that follow.

Hapa Mkindani, mtaa ulioko sehemu ya magharibi ya Dar es Salaam kuna nyumba moja ya kukodisha. Nyumba hii ina vyumba viwili vya kulala na sebule moja kubwa. Chumba cha maakuli kiko karibu na sebule. Kando ya sebule kuna jikoni kubwa ambalo liko wazi. Ndani ya nyumba kuna vyoo viwili na mabafu mawili. Nyumba ina maji ya bomba na umeme. Kuna chumba kimoja kidogo ambacho kinaweza kutumika kama ofisi au maktaba. Nyumba hii iko katika barabara ya Kimambo. Mtaa huu ni salama sana. Pia uko karibu na maduka na soko la wazi la Kariakoo. Kuna madhehebu mengi katika eneo hili. Eneo hili ni safi. Kodi ya nyumba ni shilingi milioni mbili na laki tano kila mwezi. Nyumba hii iko tayari, kwa hivyo unaweza kuhamia katika nyumba hii wakati wowote. Piga simu kwa nambari hii: +255 780 789 8970, iwapo una maswali ya ziada kuhusu nyumba hii.

1. Nyumba hii iko wapi?
2. Hali ya mtaa huu iko vipi?
3. Ikiwa una maswali kuhusu nyumba hii unahitaji kufanya nini?
4. Kuna vitu gani vingine karibu na nyumba hii?
5. Kodi ya nyumba hii ni shilingi ngapi kila mwezi?



## Zoezi B

Joseph wants to learn more about an apartment in Nairobi that his friend's parents occasionally rent out. It sounds perfect for a trip he and some classmates want to take during the mid-semester break. Read Joseph's email to his friends and answer the questions that follow.



Hamjambo rafiki,

Ninatumai mko salama na pia mko tayari kwa safari ya kwenda Nairobi. Ningependa kuwajulisha zaidi kuhusu nyumba ambayo tunaweza kukodi wakati wa safari yetu mjini Nairobi. Nyumba hii iko katika mtaa wa Westlands ambao uko kilomita 5 kutoka mji wa Nairobi. Nyumba hii ina vyumba vinne vya kulala. Pia ina chumba cha burudani na chumba cha maombi ambacho pia kinaweza kutumika kwa masomo. Nyumba hii iko katika ghorofa ya pili na ina mandhari mazuri sana ya mto na msitu. Sakafu ya nyumba ni ya mbao, dari katika kila chumba ni la jasi. Pia kila chumba kina taa za mtindo wa kisasa. Mandhari mazuri ya mji wa Nairobi yanaweza kuonekana kupitia kwenye madirisha ya sebule na ya vyumba vya kulala. Jikoni ni la wazi na lina baa la vyakula vya asubuhi, sinki ambayo ina beseni mbili, mashine ya kuosha vyombo na kifaa cha kuchuja maji, kipepeo, tanuri, maikrowevu na kabati la vyakula. Vifaa vingine katika eneo hili ni jenereta, kisima, mtambo wa kuchemsha maji kwa kutumia jua, na chumba cha mazoezi. Kodi ya nyumba kila mwezi ni shilingi elfu mia mbili. Kwa sababu tutakuwa na wapangaji kwa muda, huhitaji kulipa malipo ya amana ya usalama. Tafadhali nijulisheni maoni yenu kuhusu nyumba hii. Tutajadili zaidi baadaye.

Wenu,  
Joseph.

1. Nyumba ambayo Joseph na wenzake wangependa kukodi iko katika mtaa gani mjini Nairobi?
2. Kodi ya nyumba hii ni shilingi ngapi kila mwezi?
3. Kwa nini wapangaji hawahitaji kulipa amana ya usalama?
4. Nyumba hii ina aina gani ya sakafu na dari?
5. Kuna vifaa gani katika jikoni?
6. Kuna vitu gani kati eneo la nyumba hii ambavyo vinatumika na jamii nzima?



### Zoezi C

Read the dialogue between Amina and Bakari and answer the questions that follow.



**Amina:** Uhali gani Bakari?

**Bakari:** Salama tu. Habari za wikendi?

**Amina:** Wikendi ilikuwa nzuri. Nilikuwa na shughuli nyingi za kuhama.

**Bakari:** Ulihamia wapi?

**Amina:** Nilihama kutoka kwa apatmenti yangu. Nilipata nyumba ya kukodi karibu na chuo kikuu. Ninataka kukaa karibu na chuo kwa sababu kuna changamoto nyingi za msongamano wa magari kila asubuhi na jioni, kwa hivyo mimi hupoteza muda mwingi barabarani.

**Bakari:** Umehamia katika mtaa gani?

- Amina:** Nimehamia katika mtaa wa Kahawa Sukari kwenye apatmenti za Mitula. Unazifahamu?
- Bakari:** Hapana siufahamu mtaa wa Kahawa Sukari. Je, apatmenti iko vipi?
- Amina:** Apatmenti ina sebule yenye nafasi kubwa, kuna sehemu ya maakuli, jikoni kubwa nzuri ambayo ni rahisi kusafisha. Kuna makabati mengi ya kuweka vitu na msala kwa wageni.
- Bakari:** Kweli nyumba hii inapendeza sana. Chumba chako cha kulala kikoje?
- Amina:** Ni chumba kikubwa ambacho kina roshani ndogo. Pia kuna sehemu mbili za kugesha magari, maji ya kuosha na ulinzi mkali kila wakati kwenye wiki.
- Bakari:** Ni nyumba kubwa sana! Kodi ni pesa ngapi kila mwezi?
- Amina:** Kila mwezi nitalipa shilingi elfu hamsini.
- Bakari:** Bei ghali sana!
- Amina:** Ndiyo ni kwa sababu nyumba iko karibu na chuo na pia kuna vitu vingi muhimu karibu kama vile soko, maduka mengi, misikiti mingi, makanisa mengi, shule za msingi na sekondari na sehemu za starehe.
- Bakari:** Ni kweli kabisa.

1. Kwa nini Amina alihamia kwenye apatmenti ambayo iko karibu na chuo chake?
2. Amina alihamia katika mtaa gani?
3. Jikoni ya Amina ina sifa gani?
4. Kodi ya nyumba ya Amina ni pesa ngapi kila mwezi?
5. Kwa nini kodi ya nyumba ya Amina ni ghali?
6. Hali ya ulinzi iko vipi katika apatmenti anamoishi Amina?
7. Mtaa wako na apatmenti yako ina sifa gani?



### Zoezi D

Listen to the advertisement of a house for rent and answer the questions that follow.

1. Je, nyumba hizi za kukodishwa au kununuliwa ziko wapi?
2. Kodi ya nyumba ni pesa ngapi kila mwezi?
3. Tangi la maji linaweka kiwango kipi cha maji?
4. Nyumba ina vyumba vingapi vya kulala?
5. Kuna huduma gani kwa watu ambao wanaishi katika nyumba hizi?
6. Nyumba hii ina sifa gani?



## Zoezi E

Read the phone conversation between a leasing agent and a Kiswahili student, Fola, who has decided to rent a house for the remainder of her study abroad program. Then, answer the questions that follow.

**Ajenti:** Hujambo dada?

**Fola:** Sijambo. Habari za leo?

**Ajenti:** Salama sana na wewe je?

**Fola:** Niko salama kabisa. Ningependa kukodi nyumba kwa muda wa miezi sita. Je, kuna nyumba?

**Ajenti:** Ndiyo, nina nyumba mbili za kukodisha, na pia kuna apatmenti. Apatmenti ina vitu vya nyumba lakini nyumba hazina vitu. Ungependa kukodi aina gani ya nyumba?

**Fola:** Ningependa apatmenti yenye vyumba viwili vya kulala, mabafu mawili, vyoo viwili, jikoni, sehemu ya kuoshea nguo na chumba cha ziada cha mfanyakazi.

**Ajenti:** Tuna apatmenti nzuri ambayo unaweza kukodi. Kila apatmenti ina chumba cha ziada cha mfanyakazi ambacho kina msala.

**Fola:** Sawa. Je, mnatoa huduma gani kwa wapangaji?

**Ajenti:** Kuna huduma za ulinzi katika milango miwili ya eneo hili la makazi. Walinzi hukagua na kuelekeza wageni wanaoingia kwenye makazi baada ya wapangaji kutoa idhini. Kuna huduma za kusafisha maeneo ambayo yanatumiwa na watu wengi kama vile (ngazi na ua). Pia, kuna huduma za kukata nyasi na kuzizoa. Pia tunachukua takataka zote na kuzipeleka katika eneo la kukusanya takataka mjini.

**Fola:** Sawa. Asante kwa maelezo hayo. Je, ni nani ana gharamia ada za maji na umeme?

**Ajenti:** Ada za maji, takataka na ulinzi hujumuishwa katika malipo ya kodi ya kila mwezi. Kwa hivyo mpangaji anahitaji kugharamia umeme tu.

**Fola:** Kodi ya kila mwezi ni ngapi?

**Ajenti:** Kila mwezi kodi ni shilingi elfu themanini na tano. Utahitaji pia kulipa amana ya usalama ambayo ni kodi ya miezi miwili.

**Fola:** Ala! Bei ni ghali sana. Je, ninaweza kulipa amana ya usalama ya mwezi mmoja badala ya miezi miwili?

**Ajenti:** Kwa kawaida unahitaji kulipa kodi ya miezi miwili. Nitamwuliza meneja iwapo inawezekana wewe kufanya hivi. Nitakupigia simu kukueleza uamuzi wake. Je, ungependa kuingia kwenye nyumba lini?

**Fola:** Ningependa kuingia mwanzo wa mwezi ujao. Lakini pia ningependa kuona nyumba ambazo ziko wazi.

**Ajenti:** Bila shaka unaweza kuja sasa kuangalia nyumba ambazo ziko wazi.

**Fola:** Sawa. Nitakuja baada ya saa moja.

**Ajenti:** Sawa, nipigie simu iwapo utahitaji maelekezo ya kufika huku.

1. Fola angependa kukodi nyumba au apartmenti?
2. Je, apartmenti zote za ajenti zina vitu vya nyumba?
3. Wapangaji katika mtaa huu wanapata huduma gani?
4. Fola angependa kuingia kwenye nyumba lini?
5. Fola atahitaji kulipa amana ya usalama ya pesa ngapi?
6. Ni ada gani ambazo hujumuishwa kwenye malipo ya kodi?
7. Walinzi hufanya nini kwenye milango mikuu ya makazi?



### Zoezi F

During the break between semesters, Shamila would like to visit Nairobi for a few weeks. To see if this would be possible, she calls a leasing agent there to ask about possible accommodation options. Listen to their conversation and answer the questions that follow.

1. Nyumba ambayo Shamila anataka kukodi ina sehemu gani?
2. Kodi ya nyumba ya chumba kimoja ni ngapi kila mwezi?
3. Nyumba hii ina huduma gani?
4. Nyumba hii iko katika ghorofa ya ngapi?
5. Je, Shamila atahitaji kutia saini kwenye mkataba wa upangaji?



### Zoezi G

You would like to find accommodation for the weekend and you come across the advertisement below. Review the information with a classmate and decide if you would like to rent the house. Be prepared to share your decision with the class.

#### **Nyumba ya kukodisha mwenyeji ni Farah**

Wageni 4, vyumba 2 vya kulala, vitanda 2, mabafu 2.

#### **Nyumba nzima**

Utamiliki nyumba kama yako mwenyewe.

#### **Usafishaji wa hali ya juu**

Mwenyeji huyu amejizatiti kufuata mchakato wa hatua 5 za Airbnb wa kufanya usafi wa hali ya juu.

Wageni mara nyingi hutafuta makazi haya maarufu.

Nyumba ni ya kisasa na ya kifahari katika kitongoji salama huko Masaki. Kuna sehemu tulivu ya kupumzika ndani na nje ya bwawa. Nyumba iko karibu dakika tano kutoka pwani ya Slipway na kilabu cha Yatch. Inapatikana kwa urahisi na iko

karibu sana na baa maarufu, mikahawa, maduka makubwa na maeneo ya burudani. Nyumba hii ina sebule, chumba cha maakuli, vyumba viwili vya kulala, na mabafu mawili.

**Nyumba hii ina vitu vifuatavyo:** jiko, Wi-Fi, eneo la kugesha gari bila malipo, bwawa, televisheni, kambarau, mashine ya kufua nguo, kiyoyozi, kikaushaji nywele, taulo, mashuka, sabuni, shashi, viango vya nguo, pasi, kengele ya moshi, kizima moto, vifaa vya huduma ya kwanza, dawati, meza, viti, nafasi ya kompyuta na chumba cha mazoezi.



## Zoezi H

Assume your study abroad program has ended but that you are staying on in Tanzania to work on a research project. However, your lease is up and so you will need to rent a different house or apartment for the next four months. Prepare four to six questions that you might ask the leasing agent about a potential property.

### Sarufi: *-ote (all/entire/whole)*

In the course of this unit, you have seen a few uses of the word *-ote*, which corresponds roughly to the English words “all/entire/whole.”

Katika nyumba ya Bibi Farida, vyumba **vyote** vya kulala ni vya rangi ya kijani.  
*In Mrs. Farida's house, **all** the bedrooms are green.*

Je, apatimenti **zote** zina vitu vya nyumba?  
*Do **all** apartments have household items?*

Tunachukua takataka **zote** na kuzipeleka katika eneo la kukusanya takataka mjini.  
*We take **all** the garbage to the city garbage collection point.*

As you can see from the examples below, *-ote* is used to indicate the entirety of something (singular) or all of something (plural).

*(You cannot use -ote in singular form with the M-WA class.)*

wanyama wote

***all** the animals*

kiti chote

*the **whole/entire** chair*

viti vyote

***all** the chairs*

nyumba yote

*the **whole/entire** house*

nyumba zote

***all** the houses*

The use of *-ote* corresponds to the class of the noun being modified.

Wasichana **wote** wanasoma.

***All** the girls are studying.*

Kitabu **chote** kina maji.

*The **whole** book is wet.*

Vitabu vyote vina maji.

***All** the books are wet.*

Nyumba **yote** imeoshwa.

*The **whole** house has been cleaned.*

Nyumba **zote** zimeoshwa.

***All** the houses have been cleaned.*





## Zoezi I

Fill in the blanks with the correct forms of *-ote*. Be sure to pay attention to the class of the noun that *-ote* modifies.

1. Mama alinunua vyakula \_\_\_\_\_ kutoka soko la wazi la Mwembe Tayari.
2. Amina alisafisha nyumba \_\_\_\_\_. Zililikuwa safi sana.
3. Kalamu \_\_\_\_\_ za mwalimu ni za rangi nyekundu.
4. Visu vyake \_\_\_\_\_ vimepoteza makali.
5. Watoto \_\_\_\_\_ hulala saa mbili na nusu za usiku.
6. Simu \_\_\_\_\_ za wanafunzi zitabaki ofisini wakati wa kufanya mtihani.
7. Rafiki zangu \_\_\_\_\_ wanasema Kiswahili.
8. Kitabu chake \_\_\_\_\_ kiliharibiwa na mvua.
9. Tulienda mkahawani na familia \_\_\_\_\_.
10. Shalima anapenda wanyama \_\_\_\_\_.



## Zoezi J

Write ten sentences using *-ote* to describe things in your house or apartment. Be prepared to report back to the class.



## Zoezi K

Pretend that you are packing your house to move. Ask your classmates five questions about the things you have packed.

### **Example:**

Kwa nini umepanga elektroniki zote mezani?

### **Sarufi: -o-ote (any)**

In the previous grammar section, you learned that *-ote* is used to indicate the entirety of something (singular) or all of something (plural). Another adjective that works in a similar way is *-o-ote*, which corresponds roughly to the English word “any.” Here are a few examples that we have seen:

Nitaondoka baada ya nusu saa. Unahitaji kitu **chochote**?  
*I will leave in half an hour. Do you need **anything**?*

Nyumba hii iko tayari, kwa hivyo unaweza kuhamia ndani wakati **wowote**.  
*This house is ready, so you can move in at **any** time.*

Like *-ote*, *-o-ote* corresponds to the class of the noun being modified. But in the case of *-o-ote* the marker for the corresponding class is used twice.

Mwalimu yeyote anaweza kutufundisha.  
*Any teacher can teach us.*

Walimu wowote wanaweza kutufundisha.  
*Any of the teachers can teach us.*

Ninaweza kuketi kwenye kiti chochote.  
*I can sit on any seat.*

Tunaweza kuketi kwenye viti vyovyote.  
*We can sit on any seats.*

Sijui kama nyumba yoyote itajengwa.  
*I don't know if any house will be built.*

Hatujui kama nyumba zozote zitajengwa.  
*We don't know if any houses will be built.*



## Zoezi L

Fill in the blanks with the correct forms of *-o-ote*. Be sure to pay attention to the class of the noun that *-o-ote* modifies.

1. Ningependa kukodisha apartmenti \_\_\_\_\_.
2. Nikienda ofisini nitahudumiwa na mfanyakazi \_\_\_\_\_.
3. Vitabu \_\_\_\_\_ vya fasihi ni muhimu kwa kuboresha lugha.
4. Anapenda simu \_\_\_\_\_ za kisasa.
5. Sipendi chumba \_\_\_\_\_ ambacho hakina madirisha.
6. Wanafunzi \_\_\_\_\_ chuoni wanaweza kutumia maktaba.
7. Rafu \_\_\_\_\_ za vitabu zitanifaa kwa apartmenti yangu mpya.
8. Mama anaweza kunisaidia na vyombo \_\_\_\_\_ vya jikoni.
9. Matunda \_\_\_\_\_ ni mazuri kwa afya.
10. Wageni wanaweza kulala katika chumba \_\_\_\_\_.



## Zoezi M

You have been packing all day for your move to a new apartment. A friend has just arrived with a home-cooked dinner to eat before they help you finish packing. Role-play the scenario using *-ote* and *-o-ote* to get the table set so that you can eat.

### **Examples:**

Je, tuna nyuma zozote?  
*Do we have any forks?*

Hapana, hatuna nyuma zozote. Nimepanga nyuma zote.  
*No, we do not have any forks. I have packed all the forks.*

## **Cultural Explorations**

Multi-family properties are common in East Africa, with siblings building homes on family homesteads to retain close connections. People living in urban areas are thus more likely to rent with an expectation that they will return to their homesteads on a regular basis. Many retirees also return permanently to be close to their families for support and care in their old age. Property in urban areas has also been prohibitively expensive for many, especially with high interest rates and short repayment terms on mortgages.

In Kenya, most leasing agreements function on a month-to-month basis with a security deposit and one month's rent paid when making the initial agreement; newer apartment complexes may, however, require long-term leases and a larger portion of the rental payment (perhaps several months) due in advance. In Tanzania, renters may even be required to pay a security deposit and the rent for the entire leasing period before gaining access to the property. It is common to have a rental agreement based on an oral agreement rather than a signed lease.

Rental prices include the costs of most utilities (e.g., electricity, internet, water, etc.) as well as any maintenance costs to keep the apartment in working order. Rent may also include access to shared amenities like a pool or a gym. Properties are typically unfurnished, but furnished properties are gaining popularity in larger urban areas. Services like Airbnb are also growing in popularity for short-term rentals, with a large number of advertisements appearing in English.

## **Cultural Reflections**

With a classmate or in a small group, discuss the cultural information you have just read by answering the questions that follow.

1. What are the typical lease agreements like where you live? What are some of the pros and cons of paying rent on a month-to-month basis? What are some of the pros and cons of paying the entirety of the rent before moving in? Do you have a preference?
2. Is it common in your culture to rent or to own a home? Is it common for people to have multiple properties? If so, what are some typical examples? How does this compare to the use of the family homestead by East Africans living in cities?
3. How important is the family home in your region or culture? How is it similar or different to the importance of the family homestead in East African culture? Do you think that this importance, or perhaps lack of importance, will change in the coming years? Why or why not?



## Zoezi N

Read the advertisement below and then answer the questions that follow.

### *Makazi ya Malo*

Hii nyumba ni maridadi na moja ya aina yake iliyoko katikati ya Mikocheni. Makazi ya Malo yana muundo mzuri wa ndani ambao unawafaa watu wengi. Nyumba iko katikati ya mji mpya wa Ukoko. Ni makazi mazuri kwa wafanyabiashara, familia na watu binafsi ambao wanataka kulitembelea jiji kwa urahisi.

#### **Sehemu**

Nyumba hii ni mpya na ina sakafu pana, dari ndefu, na madirisha makubwa ambayo hutoa mwangaza mwingi. Kuna huduma za bure za Wi-Fi.

Jikoni mna vifaa vifuatavyo — maikrowevu, birika la umeme, jiko la umeme, friji ya milango miwili, vyombo vya kahawa na chai. Sebule ina vigae safi sana, eneo la kukaa ambalo lina sofa mpya kabisa, meza, runinga na satelaiti. Vyumba vya kulala viko katika sehemu ya juu ambayo ina kitanda kikubwa ambacho kina godoro lenye starehe, mablanketi, shuka, na mito safi. Kila chumba cha kulala kina bafu na choo. Kila msala una milango mikubwa na vioo. Katika bafu kuna taulo nyingi ambazo ni safi. Kuna pasi na bodi ya kupiga pasi.

Hakuna uvutaji wa sigara unaoruhusiwa ndani ya nyumba ya wageni. Unaweza kuvuta sigara kwenye roshani. Hakuna wanyama wanaoruhusiwa kwenye nyumba na hakuna kufanya karamu. Huduma za umeme ni ghali sana katika mji wa Dar es Salaam, kwa hivyo ukikaa zaidi ya siku mbili utatozwa shilingi elfu kumi zaidi kwa siku moja.

Unaweza kupika vyakula vyako mwenyewe. Jikoni, unaweza kuhifadhi chakula kwenye friji, unaweza pia kupasha moto chakula chako kwa kutumia maikrowevu, na kutengeneza vitafunio vyepesi. Huhitaji kupika nyumbani. Ni bora, kwenda kwenye mikahawa iliyo karibu kama vile Rose Garden, Bustani ya Hekima na Grill ya Mwenge.

Mwenye nyumba yuko tayari wakati wa wikendi kukuonyesha maeneo mazuri yaliyo karibu na nyumba kama vile pwani za Mbalamwezi na Velisa. Maeneo mengine ya kutembelea ni uchoraji maarufu wa Tinga-Tinga na soko la Makonde ambako kuna sanamu za mbao. Kituo cha mwisho cha ziara ni Pwani ya Koko ambayo iko dakika chache kutoka kwenye nyumba hii. Pwani hii imejaa wauzaji wa vyakula mbalimbali vya eneo hili.

1. Nyumba hii inawafaa wageni wa aina gani?
2. Kuna huduma gani za bure kwa wapangaji kwenye nyumba hii?
3. Vitu gani ambavyo haviruhusiwi katika nyumba hii?
4. Kuna sehemu gani za vyakula karibu na nyumba hii?
5. Kwa nini mwenyeji huwatoza wapangaji shilingi elfu kumi wakati wanapokaa kwenye nyumba zaidi ya siku mbili?
6. Mwenyeji hujitolea kufanya nini na wapangaji wanapozuru nyumba hii mara ya kwanza?

7. Ni maeneo gani ambayo wageni wanaweza kutembelea ambayo yako karibu na nyumba hii?
8. Je, wapangaji wanaruhusiwa kupika vyakula katika nyumba hii?
9. Je, iwapo unatafuta nyumba ya kukodisha ungechagua Makazi ya Malo? Kwa nini?
10. Kuna usawa gani kati ya Makazi ya Malo na mahali unapokaa?



### **Zoezi O**

Work with a classmate to create a role-play based on *Zoezi N*. Call your partner (the leasing agent) to inquire about a possible tour of the rental and to ask any additional questions you may have about the house (e.g., cost, rental agreement procedures, the neighborhood, amenities, etc.).



### **Zoezi P**

Imagine that you have been awarded a fellowship to study at MS Center for Training and Development in Arusha for the year. Search online for available apartment options in Arusha and select one as your choice. Prepare a short presentation that describes, in detail, the interior and the exterior of the apartment, the items in each room, the neighborhood, and the amenities available to the renters in the apartment complex. Include details on the cost of renting, for example the rental deposit, utilities, et cetera.

Be prepared to answer questions about your presentation and to ask others about their presentations.

## Key Vocabulary

### Nouns

<b>chumba kikuu cha kulala</b>	master bedroom
<b>dhamana</b>	deposit
<b>dhamana ya usalama</b>	security deposit
<b>fomu</b>	form
<b>fomu ya maombi</b>	application form
<b>funguo</b>	keys
<b>gesi</b>	gas
<b>haki</b>	fairness; justice; right
<b>hali</b>	condition
<b>huduma</b>	services
<b>huduma za kukusanya taka</b>	garbage collection services
<b>jasi</b>	gypsum
<b>kambarau</b>	elevator; lift
<b>kengele ya moshi</b>	smoke alarm
<b>kiango cha nguo</b>	clothing accessories
<b>kifaa</b>	equipment
<b>kikaushaji nywele</b>	blow dryer
<b>kitambulisho</b>	identification
<b>kizima moto</b>	fire extinguisher
<b>kodi; malipo ya nyumba</b>	rent
<b>kufuli za milango</b>	door locks
<b>makubaliano</b>	agreement
<b>malalamiko</b>	complaints; grievances
<b>malipo</b>	payment
<b>mandhari</b>	landscape; view
<b>marekebisho</b>	repairs
<b>masharti</b>	rules
<b>mbao</b>	wood
<b>mita</b>	meter
<b>mkataba wa upangaji</b>	lease agreement
<b>mkodishaji; mpangaji</b>	tenant; renter
<b>mwenye nyumba; mpangishaji</b>	landlord; leaser
<b>nakala</b>	copy; replica
<b>ploti</b>	plot of land
<b>ripoti</b>	report; information
<b>saini</b>	signature
<b>saruji</b>	cement
<b>taa za usalama</b>	security light
<b>taarifa</b>	information; notice
<b>taka; takataka</b>	garbage
<b>tatizo</b>	problem; issue
<b>uharibifu</b>	destruction
<b>ukarabati</b>	renovation; redecoration
<b>ukubwa</b>	size
<b>ukuta wa mzunguko</b>	perimeter wall
<b>ulinzi</b>	protection
<b>umeme</b>	electricity

**usalama** security  
**wakala** agent (leasing agent)  
**walinzi; bawabu** security guards

### Verbs

**-arifu** to notify; to inform  
**-hama** to move  
**-hamia** to move in  
**-haribu** to destroy; to ruin  
**-ingia** to enter; to go in  
**-karabati** to repair; to redecorate  
**-kukodi** to rent  
**-lalamika** to complain; to protest  
**-linda** to care for  
**-lipa** to pay  
**-lipa dhamana** to pay a deposit  
**-ondoa** to remove  
**-ongeza** to add  
**-paka** to paint  
**-panga** to rent; to arrange; to plan  
**-rekebisha** to repair; to fix; to assemble  
**-ripoti** to report  
**-sababisha** to cause; to make happen  
**-tengeneza** to make  
**-toka** to exit  
**-vunja** to break  
**-vunja mkataba** to break agreement  
**-vunjika** to break; to destroy; to damage

### Key Phrases

**Kodi ya nyumba ni pesa ngapi?** How much is the rent?  
**Kuna huduma gani kwenye nyumba?** What services are provided at the house?  
**Kuna mandhari gani kwenye eneo hili?** What is the view from the place?  
**Kuna sehemu nyingi za vyakula.** There are many restaurants.  
**Kuna sheria zozote kuhusu matumizi ya nyumba?** Are there any rental restrictions?  
**Nyumba haina vitu vyovyote.** The house is not furnished.  
**Nyumba ina vitu gani?** What things are in the house?  
**Nyumba ina vitu vyote.** The house is fully furnished.  
**Unaweza kutembelea maeneo gani karibu na nyumba hii?** What places can you visit around this house?

## Sources

### 4.1 Nyumba ya familia yangu pokezi

- "Addison Place at Boca Raton" by Jasmine Villa is licensed under CC BY 2.0. Modifications by Jonathan Perkins. Last accessed 9/16/2021. <https://flickr.com/photos/addisonplace/2832996979/>
- "400 W. Kenneth Rd. Floorplan" by Kendyl Young is licensed under CC BY 2.0. Modifications by Jonathan Perkins. Last accessed 9/16/2021. <https://flickr.com/photos/kendylyoung/7652795482>
- "Living-room view" by jinkazamah is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 5/10/21. <https://www.flickr.com/photos/jinkazamah/4479975740>
- "10302 Sterling Springs Rd Dining Room" by KairosPhotography is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 5/10/21. <https://www.flickr.com/photos/kairosphoto/4512146374>
- "Kitchen" by Michael Kroepfl is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 2/23/21. <https://www.flickr.com/photos/22695964@N00/5328898227/>
- "Bedroom" by ybsme is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 2/23/21. <https://www.flickr.com/photos/basibanget/4472973744/>
- "Family Bathroom" by Gareth Simpson is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 2/23/21. <https://www.flickr.com/photos/xurple/119384909/>
- "Porches on the Point" by nola.agent is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 5/10/21. [https://www.flickr.com/photos/nola\\_agent/2660543934/](https://www.flickr.com/photos/nola_agent/2660543934/)
- "Laundry room" by Matthew Gosselin is licensed under CC BY ND 2.0. Last accessed 5/10/21. <https://www.flickr.com/photos/mattgosselin/6977912004>
- "Garage Doors Carriage House Patina Green" by Cary Peterson is licensed under CC BY ND 2.0. Last accessed 5/10/21. <https://www.flickr.com/photos/birdies100/2111021523/>
- "Floorplan" by Kendyl Young is licensed under CC BY 2.0. Modifications by Jonathan Perkins. Last accessed 10/28/2021. <https://flickr.com/photos/kendylyoung/5861824570>
- "440 49<sup>th</sup> Street" by Jordan Klein is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 9/30/21. <https://www.flickr.com/photos/jordanklein/23091234851>
- "Tazara Rail" by Richard Stupart is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 10/28/2021. <https://www.flickr.com/photos/richardstupart/4274075599>
- "Nairobi skyline from Uhuru Park » by Fiona Graham / World Remit is licensed under CC BY SA 2.0. Last accessed 9/16/21. <https://www.flickr.com/photos/worldremit/33301983500>

### 4.2 Kuna nini katika vyumba mbali mbali?

- "Living Room" by Jordan Klein is licensed under CC BY 2.0 Generic. Last accessed 10/28/2021. <https://www.flickr.com/photos/jordanklein/22661651567>
- "Kitchen" by Jordan Klein is licensed under CC BY 2.0 Generic. Last accessed 10/28/2021. <https://www.flickr.com/photos/jordanklein/22661615398>
- "Master Bedroom" by Jordan Klein is licensed under CC BY 2.0 Generic. Last accessed 10/28/2021. <https://www.flickr.com/photos/jordanklein/23080022135>
- "Dining Room" by Jordan Klein is licensed under CC BY 2.0 Generic. Last accessed 10/28/2021. <https://www.flickr.com/photos/jordanklein/22687741109>
- "Access to electricity (% of population) - Tanzania, Kenya" by the World Bank is licensed under CC BY 4.0. Last accessed 10/28/2021. [https://data.worldbank.org/indicator/EG.ELC.ACCS.ZS?end=2019&locations=TZ-KE&name\\_desc=false&start=1992&view=chart](https://data.worldbank.org/indicator/EG.ELC.ACCS.ZS?end=2019&locations=TZ-KE&name_desc=false&start=1992&view=chart)



### 4.3 Nje ya nyumba

- “Interior Design 3d Rendered 3d Rendering Living Room” is in the public domain. Last accessed 7/29/2021. <https://www.maxpixel.net/Interior-Design-3d-Rendered-3d-Rendering-Living-Room-5570451>
- “Kenya - Typical village houses” by Marcel Oosterwijk is licensed under CC BY SA 2.0. Last accessed 1/6/2022. <https://www.flickr.com/photos/wackelijmrooster/4992353297>
- “Decorative House, Tanzania” by Rod Waddington is licensed under CC BY SA 2.0. Last accessed 1/6/2022. [https://www.flickr.com/photos/rod\\_waddington/10165518704/](https://www.flickr.com/photos/rod_waddington/10165518704/)
- “Kabete Post Office -3” by Richard Portsmouth is licensed under CC BY SA. Last accessed 11/1/2021. <https://www.flickr.com/photos/62358811@N02/6203197460>

### 4.4 Mtaa na Ujirani

- “Al Haashimy Academy” by Francisco Anzola is licensed under CC BY 2.0. Last accessed 1/26/21. <https://www.flickr.com/photos/fran001/51301553866>
- “Kenya Gated Community” by Brenda Wawire is licensed under CC BY 4.0.

# Appendices

## Noun Classes

Noun Class		Subject prefix	Adj. prefix	Object prefix (5.1)	Poss. prefix (4.1)	Amba- and o- of reference (2.4)
M-WA	sing.	a-	m-	-mw-	w- (y-)	-ye-
	pl.	wa-	wa-	-wa-	w- (z-)	-o-
KI-VI	sing.	ki-	ki-	-ki-	ch-	-cho-
	pl.	vi-	vi-	-vi-	vy-	-vyo-
N-N	sing.	i-	n-	-i-	y-	-yo-
	pl.	zi-	n-	-zi-	z-	-zo-
JI-MA	sing.	li-		-li-	l-	-lo-
	pl.	ya-	ma-	-ya-	y-	-yo-
M-MI	sing.	u-	m-	-u-	w-	-o-
	pl.	i-	mi-	-i-	y-	-yo-
U-U		u-	m-	-u-	w-	-o-
U-ZI	sing.	u-	m-	-u-	w-	-o-
	pl.	zi	n-	-zi-	z-	-zo-
KU-KU		ku-	ku-	-ku-	kw-	-ko-
PA-PA		pa-	pa-	-pa-	p-	-po-
MU-MU		m-	m-		mw-	-mo-

# Verb Conjugation

## Affirmative

Subject Pronoun	Present -na-	Present Perfect -me-	Past -li-	Future -ta-	Habitual -hu-
mimi	ninasoma	nimesoma	nilisoma	nitasoma	husoma
wewe	unasoma	umesoma	ulisoma	utasoma	husoma
yeye	anasoma	amesoma	alisoma	atasoma	husoma
sisi	tunasoma	tumesoma	tulisoma	tutasoma	husoma
nyinyi	mnasoma	mmesoma	mlisoma	mtasoma	husoma
wao	wanasoma	wamesoma	walisoma	watasoma	husoma

## Verb Negation

Subject Pronoun	Present Ø (final vowel to -i)	Pres. Perfect -ja-	Past -ku-	Future -ta-	Habitual huwa + neg. present
mimi	sisomi	sijasoma	sikusoma	sitasoma	huwa sisomi
wewe	husomi	hujasoma	hukusoma	hutasoma	huwa husomi
yeye	hasomi	hajasoma	hakusoma	hatasoma	huwa hasomi
sisi	hatusomi	hatujasoma	hatukusoma	hatutasoma	huwa hatusomi
nyinyi	hamsomi	hamjasoma	hamkusoma	hamtasoma	huwa hamsomi
wao	hawasomi	hawajasoma	hawakusoma	hawatasoma	huwa hawasomi